SportPesa
TZS. 642,668,240
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



## DENI la Taifa lapaa kufikia trilioni 64.5/-

UKURASA 3




UKURASA 11

# Nipashe

Ijumaa Novemba 5, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580755

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

## Shahidi kesi ya Mbowe aomba radhi kizimbani

UKURASA 2

# Sakata la machinga latinga bungeni



Wafanyabiashara wadogo maarufu Machinga, wakiendelea na shughuli zao kama kawaida kwa staili ya kutandika chini bidhaa zao katika eneo lisiloruhusiwa la Mwenge, Manispaa ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam jana, licha ya serikali kuondoa vibanda vyao katika maeneo hayo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

**KAMATI** ya Bajeti yapendekeza mambo manne kutafuta suluhu ya kudumu... *Endelea ukurasa wa 2*



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akipiga makofi na Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulika na masuala ya Jinsia na Uwezeshaji wa Wanawake (UN WOMEN), Hodan Addou (wapili kushoto), baada ya kuzindua Kampeni ya "HeforShe", jijini Zanzibar jana. Wengine ni Mke wa Rais wa Zanzibar, Mama Mariam Mwinyi, Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui (kulia) na Mwakilishi Mkaazi wa Umoja wa Mataifa (UN) Tanzania, Zlatan Millisic. **PICHA: IKULU**

UKURASA WA 3

### MWINYI ASIFU UTENDAJI WATEULE WANAWAKE

RAIS wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema viongozi wanawake aliowateua kuwapa nafasi za uongozi katika serikali anayoiongoza wanafanya vizuri kuliko...

UKURASA WA 3

### BUNGE LATAKA TOZO KATIKA DARAJA LA SELANDER

BUNGE limependekeza magari yatakayopita katika Daraja Jipya la Selander linalojengwa mkoani Dar es Salaam yalipie ushuru kama inavyofanyika...

UKURASA WA 4

### SABAYA ASHINDWA TENA KUFIKA KORTINI

HALI ya afya ya aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, imeendelea kuwa tete baada ya kushindwa kufika mahakamani kwa mara nyingine...

## Wafanyabiashara Tanzania, Uganda kujadiliana fursa bomba la mafuta

UKURASA 2

MICHEZO MAKAME AMWOMBA RADHI KAPOMBE KWA RAFU MBAYA UK.20

MAONI, KATUNI UK.6




Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF), Francis Nanai (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu maandalizi ya kongamano la gesi na mafuta kati ya Tanzania na Uganda, litakalofanyika Novemba 25, mwaka huu. Kushoto ni Mkurugenzi wa Bodi ya TPSF, Mhandisi Ngwisa Mpembe na Balozi wa Uganda nchini Tanzania, Balozi Richard Kabonero. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Sakata la machinga latinga bungeni

**Na Gwamaka Alipipi,**
DODOMA

BUNGE limetoa mapendekezo manne kwa serikali kuhusu operesheni inayoendelea nchini ya kuwaondoa wafanyabiashara wadogo, maarufu kama machinga katika maeneo yasiyo rasmi.

Sambamba na mapendekezo hayo, bunge limeonya kuwa endapo mapendekezo hayo hayatafanyiwa kazi kutatokea mgogoro mkubwa kati ya serikali na wananchi.

Hivi sasa katika mikoa mbalimbali nchini, kumekuwa na operesheni ya kuwaondoa machinga katika maeneo yasiyo rasmi kwa biashara zao na kuwataka kwenda katika maeneo waliyotengewa, hali iliyosababisha taharuki na vurugu katika baadhi ya mikoa.

Kutokana na kuendelea kwa operesheni hiyo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kupitia kwa mwenyekiti wake, Siro Baran, imeishauri serikali mambo ambayo inapaswa kuyafanya.

Akisoma taarifa ya kamati kuhusu mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2022/23, pamoja na mapendekezo ya mwongozo wa maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/23, Baran alisema kamati inakubaliana na uamuzi wa serikali wa kuwaondoa wafanyabiashara wadogo (machinga) katika maeneo yasiyo rasmi na kupelekwa kwenye maeneo yaliyotengwa kwenye halmashauri za majiji, manispaa na wilaya.

"Hata hivyo, ikumbukwe kwamba kumekuwa na ongezeko kubwa la nguvu kazi lisiloendana na uwezo wa uchumi kuajiri. Hivyo ni wazi kwamba lazima vijana watajitafutia namna ya kupata kipato. Pia ni jukumu la serikali kuhakikisha vijana hao ambao wamelazimika kuwa machinga, wapate fursa na maeneo sahihi ya kufanya biashara," alisema Baran ambaye ni Mbunge wa Babati Vijijini.

Alisema kutoka na sakata hiyo kamati inaishauri serikali kupitia mamlaka za serikali za mitaa kutenga maeneo rasmi kwa ajili ya machinga na maeneo hayo yawe yale yanayovutia ufanyaji biashara kwa kuwekewa miundombinu ya msingi na yawe karibu na maeneo yaliyozoeleka.

Pia alisema serikali ihakikishe maandalizi ya maeneo rasmi ya biashara ya machinga pamoja na ujenzi wa miundombinu ya msingi yanafanyika katika mwaka huu wa fedha 2021/22 na kukamilika katika mwaka ujao wa fedha 2022/23, ili kuwawezesha wafanyabiashara hao kuendelea kujitafutia kipato na kutunza familia zao. Barani alisema ushauri wa tatu ni lazima serikali ifanye tathmini ya soko la ajira nchini ili kuja na mipango ya kuchochea ajira hasa kwa vijana.

Ushauri wa nne, ni lazima sasa suala la kurasimisha sekta isiyo rasmi liwe endelevu ili kuondokana na kuhamisha wafanyabiashara wadogo kila mwaka.

"Kamati inaamini yasipofanyiwa kazi mapendekezo haya tunaandaa mgogoro mkubwa kati ya Serikali na wananchi hasa hawa wafanyabiashara wadogo ambao wengi ni vijana," alisema.

## Wajadili fursa za bomba la mafuta

**Na Christina Mwakangale**

SEKTA binafsi Tanzania na Uganda, zimeandaa kongamano litakalokutanisha wafanyabiashara wa nchi hizo mbili ili kujadili na kutoa fursa za kibiashara kupitia mradi wa bomba la kusafirisha mafuta kutoka Hoima hadi Chongoleani, Tanga.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Francis Nanai, akizungumza na waandishi wa habari jana, alisema kongamano hilo litakalofanyika mkoani Dar es Salaam, litahusisha zaidi ya watu 2,000 kati yao kushiriki kwa njia ya mtandao.

Alisema lengo la kongamano ni kuwandaa Watanzania na Waganda, waliojiajiri kwenye sekta binafsi kujiandaa kuendesha miradi itakayohusiana na mradi huo ikiwamo, kampuni za uondoshaji na usafirishaji mizigo kutoka bandarini, zinazotoa huduma za hoteli na mfumo wa teknolojia wa kisasa.

"Mradi huu wa bomba lenye urefu wa kilomita 1,443 utakuwa na thamani ya uwekezaji dola za kimarekani bilioni 20, tunatarajia miradi ndani yake kwa wakazi wetu. Mkutano huu utafanyika Novemba 25, mwaka huu ni ushirikiano wa serikali mbili, Wizara ya Nishati na Wizara ya Mambo ya Nje Uganda kupitia ubalozi wake nchini," alisema Nanai. Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi Uganda (PSFU), Dk. Elly Karuhanga, alisema ushirikiano wa sekta binafsi kwa nchi mbili utawanufaisha wakazi wake hususan kweye miradi itokanayo na maliasili.

"Kwenye mkutano huu tutapanga namna maliasili za nchi zetu zinavyoweza kutunufaisha hasa kupitia gesi na mafuta. Sekta binafsi zinatakiwa kufanya kazi yake zaidi, tayari serikali imeshafanya kwa nafasi yake, sekta binafsi tusiiangushe serikali," alisema Dk. Karuhanga.

Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Godfrey Chibulunje, alisema tayari wazawa 1,011 wenye kampuni za kutoa huduma mbalimbali kwenye mradi wamejisajili ili kutoa huduma.

"Wiki mbili zilizopita walikuwa wamejisajili wenye kampuni takribani 700 hadi leo (jana) waliokwisha sajiliwa ni zaidi ya 1,000 utaona namna gani wazawa wanavyochangamkia fursa," alisema Chibulunje.

Balozi wa Uganda nchini Tanzania Richard Kabonero, alitoa wito kwa sekta binafsi kwa nchi mbili, kushirikiana ili kubadilishana uzoefu kufungua milango ya kiuchumi.

# Shahidi wa kesi ya Mbowe aomba msamaha kizimbani

**Na Kulwa Mzee**

SHAHIDI wa sita katika kesi inayomkabili Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo, Mrakibu Mwandamizi wa Polisi (SSP) Sebastian Madembwe, ameomba msamaha wakati akihojiwa kizimbani.

SSP Madembwe aliomba msamaha jana kwa makosa ya kimaandishi aliyofanya kutokana na barua ya uchunguzi kusomeka jalada la mwaka 2020 lakini majibu yake ya uchunguzi kusomeka ni jalada la mwaka 2021. Licha ya kuomba radhi, shahidi huyo alidai kuwa bastola aina ya Luger namba A5340 anayodaiwa kukamatwa nayo mshtakiwa Adamu Kasekwa, haikuwahi kusajiliwa kwa msajili wa silaha.

Madembwe alidai hayo jana katika Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi wakati akitoa ushahidi akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Pius Hillar.

Alidai kuwa Novemba 25, 2020 alipokea barua akitakiwa kufanya uchunguzi wa bastola na barua hiyo ilitoka Makao Makuu Mdogo ya Polisi, Dar es Salaam, Idara ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai.

"Nilitakiwa kuchunguza bastola iliyotengezwa na Luger namba A5340, nikajiridhisha naweza kuichunguza. niliingiza kwenye mfumo nikapata matokea hasi. "Nilibaini silaha hiyo haijawahi kusajiliwa. Matokeo yakiwa hasi huwezi kuprinti ripoti, niliandika barua ya uchunguzi kwenda kwa mwombaji nikieleza matokeo kwamba silaha haijawahi kusajiliwa,"alidai.

Shahidi aliomba barua ipokewe kama kielelezo na upande wa utetezi haukupinga, hivyo kupokewa kama kielelezo namba 10 (P 10).

Madembwe alitakiwa kusoma kielelezo hicho, akadai barua ya majibu aliandika Machi 15, 2021 ikiwa na kumbukumbu namba CD/IR/2097/2021 na barua ya kutakiwa kufanya uchunguzi ilisomeka CD/IR/2097/2020. Wakili Hillar alitaka shahidi aeleze kwa nini hizo kumbukumbu namba zinatofautiana.

"Mheshimiwa Jaji naomba msamaha kwa makosa ya kimaandishi CD/IR/2097/2021 ilipaswa kusomeka 2020 kama barua ya kuomba kufanya uchunguzi inavyosomeka CD/IR/2097/2020,"alidai.

Wakili wa utetezi, Jeremiah Mtobesya, alipinga shahidi kufanya marekebisho hayo akidai kwamba kielelezo kinatakiwa kijieleze.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Robert Kidando, alidai shahidi anaruhusiwa kufafanua yaliyomo kwenye kielelezo, hivyo hakuna kosa lililofanyika.

Jaji Tiganga alitoa mwongozo kwamba uamuzi huo waiachie mahakama, wakati inapitia ushahidi itapima ushahidi wa shahidi huyo aliyeomba msamaha kwa makosa ya kumbukumbu namba za majalada.

Kabla ya shahidi huyo kumaliza kutoa ushahidi, Wakili Mtobesya aliomba mahakama iamuru shahidi aondolewe kizimbani pamoja na ushahidi wake nusu aliotoa awali.

SSP Madembwe alipoanza kutoa ushahidi alitaja miongoni mwa majukumu yake katika Kitengo cha Udhibiti na Usajili wa Silaha kuwa ni kutoa leseni kwa raia waliokidhi vigezo vya kumiliki silaha.

Akiendelea kutoa ushahidi, Wakili Mtobesya aliinuka na kuwasilisha pingamizi akiomba mahakama imwondoe shahidi huyo pamoja na ushahidi wake kwa madai kuwa kuna ukiukwaji wa sheria.

Alidai maelezo ya shahidi huyo hayamo kwenye kumbukumbu na washtakiwa hawajapewa kabla hajaanza kutoa ushahidi wakati walipaswa kujua shahidi huyo anakuja kusema nini.

"Mheshimiwa Jaji, ushahidi wa shahidi huyu utaingia kwenye kumbukumbu bila kufuata utaratibu. Tunaomba maelekezo sababu alishaanza kutoa ushahidi kinyume na taratibu, sisi tunapendekeza aondolewe,"alidai Mtobesya.

Wakili Kidando alijibu kwamba pingamizi la upande wa utetezi halina mashiko na kwamba hoja imewasilishwa katikati ya ushahidi, hivyo shahidi aliorodheshwa na ushahidi wake ulisomwa Agosti 23 mwaka huu katika Mahakama ya Kisutu.

"Hakuna kitu kipya, hakuna haja kwa mahakama kutoa amri yoyote kuhusiana na uhalali wa ushahidi. Shahidi yuko kihalali mahakamani, tunaomba pingamizi litupwe, shahidi aendelee kutoa ushahidi,"alidai Kidando. Jaji Tiganga alipotoa uamuzi, alitupilia mbali pingamizi kwa sababu halina mashiko na kuongeza kwamba katika kumbukumbu za Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, ushahidi wa shahidi huyo ulisomwa Agosti 23, 2021.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Adamu Kasekwa, Mohammed Ling'wenya na Halfani Bwire ambao wanakabiliwa na mashtaka sita ikiwamo kula njama kufanya vitendo vya kigaidi kati ya Mei Mosi na Agosti 5, 2020.

Katika shtaka la tano, mshtakiwa Adamu anadaiwa Agosti 5, mwaka 2020 eneo la Rau alikutwa na bastola yenye namba A 5340 aina ya Luger.

HABARI KITAIFA

# Deni la Taifa lapaa hadi tril. 64.5/-

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, amesema hadi kufikia Juni, mwaka huu, deni la taifa lilikuwa limefikia wastani wa Sh. trilioni 64.497, ikilinganishwa na Sh. trilioni 56.449 kipindi cha Juni, 2020.

Amesema ongezeko hilo ni sawa na asilimia 14.3 na kwamba kati ya fedha hizo deni la nje ni Sh. trilioni 45.563 na deni la ndani ni Sh. trilioni 18.934.

Dk. Mwigulu alitoa takwimu hizo bungeni juzi wakati akiwasilisha mapendekezo ya mwongozo wa maandalizi ya mpango wa bajeti ya serikali na mapendekezo ya mapango wa maendeleo wa taifa kwa mwaka 2022/23.

Waziri Mwigulu alisema mwenendo huo wa deni umetokana na kupokewa kwa mikopo yenye masharti nafuu na ya kibiashara kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo, hususani inayochochea ukuaji wa uchumi.

Alisema pamoja na kuongezeka kwa deni la Serikali, deni hilo bado limeendelea kuwa himilivu katika muda mfupi, wa kati na mrefu.

**HALI YA SHILINGI**

Waziri Mwigulu alisema shilingi ya Tanzania imeendelea kuwa imara dhidi ya sarafu za washirika wakuu wa biashara ulimwenguni katika kipindi chote cha mwaka 2020/21.

Alisema hali hiyo imechangiwa na utulivu wa bei nchini, utekelezaji wa sera thabiti za fedha na bajeti, usimamizi imara katika soko la kubadilisha fedha za kigeni, kuimarika kwa urari wa biashara na utulivu wa bei ya mafuta katika soko la dunia.

Waziri alibainisha kuwa katika kipindi hicho, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa sh. 2,309.58, ikilinganishwa na wastani wa Sh. 2,301.30 katika kipindi kama hicho mwaka 2019/20.

"Badiliko hilo lilikuwa la kiasi cha asilimia 0.40 kwa mwaka ikilinganishwa na asilimia 0.36 katika mwaka uliopita. Kiwango hicho kilikuwa kidogo na kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi chache duniani zilizokuwa na utulivu wa kiwango cha kubadilisha fedha dhidi ya fedha za kigeni licha ya athari za ugonjwa wa virusi vya corona," alisema.

**UTEKELEZAJI BAJETI 2020/21**

Waziri Mwigulu alisema katika mwaka 2020/21, serikali imekusanya Sh. trilioni 31.280. sawa na asilimia 89.7 ya lengo.

Alisema kati ya fedha hizo Sh. trilioni 20.594 ni mapato ya ndani na Sh. trilioni 10.685 ni misaada na mikopo ya ndani na nje ya nchi.

Pia alisema serikali ilitumia Sh. trilioni 31.280 kugharamia shughuli mbalimbali ikiwamo Sh. trilioni 20.613 kwa matumizi ya kawaida na Sh. trilioni 10.667 kwa matumizi ya maendeleo.

Waziri Mwigulu alisema katika robo ya kwanza ya mwaka 2021/22, Sh. trilioni 8.419 zilikusanywa kutoka vyanzo vyote, sawa na asilimia 93.3 ya lengo la kipindi hicho.

Alisema kati ya fedha hizo, mapato ya ndani yalifikia Sh. trilioni 5.492 sawa na asilimia 89.0 ya lengo la kipindi hicho, kwamba misaada na mikopo nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo ilikuwa Sh. bilioni 534.4 sawa na asilimia 88.6 ya lengo.

Dk. Mwigulu alisema mikopo ya kibiashara kutoka katika soko la ndani ilifikia Sh. trilioni 1.220 sawa na asilimia 117.0 ya lengo la Sh. trilioni 1.043.

Kadhalika, alisema mikopo ya ndani ilivuka lengo katika robo husika kutokana na mwitikio mzuri wa wawekezaji, hususani katika hatifungani za muda mrefu.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi (kushoto), akipokea taarifa ya changamoto na mapendekezo katika Mabaraza ya Kata kutoka kwa Mwenyekiti Mwenza wa Jukwaa la Kiimani Kanda ya Ziwa, Sheikh Haruna Kichwa, jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwinyi asifu utendaji wa wateule wanawake

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema viongozi wanawake aliowateua kuwapa nafasi za uongozi katika serikali anayoiongoza wanafanya vizuri kuliko viongozi wanaume.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza katika sherehe za kumtangaza Dk. Mwinyi kuwa kinara wa kampeni ya Heforshe (Kampeni ya mwanamume na mwanamke kufikia usawa wa kijinsia) zilizoandaliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia masuala ya wanawake (UN WOMEN), zilizofanyika mjini hapa.

Alisema maendeleo yaliyopatikana Tanzania Visiwani na Tanzania Bara katika kuimarisha usawa wa kijinsia ni ya kupigiwa mfano na amekua akifanya nafasi za uteuzi za uongozi bila ya ubaguzi wa kijinsia.

Dk. Mwinyi alimteua Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi, Zena Ahmed Said na Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar, Salma Ali Hassan ikiwa ni mara ya kwanza katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, wanawake kushika nafasi hizo.

"Pia nimekuwa nikiweka mazingatio maalum ya kutoa nafasi mbalimbali za uongozi kwa wanawake wenye uwezo katika teuzi za makatibu wakuu, wakurugenzi na viongozi wa mashirika ya taasisi mbalimbali za serikali na hapa nataka niseme wanawake niliowateua hawajaniangusha hata kidogo, wanafanya kazi vizuri na niwe muwazi kabisa nafanyakazi vizuri zaidi kuliko wanaume," alisema Dk Mwinyi.

Alisema Tanzania ni mfano wa kuimarisha na kulinda katika utoaji haki kwa vitendo.

Alisema serikali itaendelea kushirikiana na Shirika la Un Women katika kutekeleza malengo na maadhimio ya kampeni hiyo ili kuimarisha usawa wa kijinsia na maendeleo ya wanawake Zanzibar.

Alisema serikali itaendelea kufanya marekebisho ya sera na sheria ili kutekeleza kwa ufanisi zaidi mikakati na mipango iliyopo katika kukabiliana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia.

"Nimekipokea na kukitumia kwa mapenzi yote cheo cha kinara cha kampeni hii mlichonitunuku...Ili kutimiza malengo na matarajio ya kampeni hii na nitapigania usawa, haki, usawa wa wanawake na wa kijinsia," alisisitiza.

Alimtaka Spika wa Baraza la Wawakilishi na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kufanya ushawishi wa kuharakisha marekebisho ya sheria ambazo bado ni kikwazo kwa maendeleo ya ustawi wa wanawake.

Naye Waziri wa Afya, Ustawi wa jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Nassor Ahmed Mazuri, alisema wakati serikali inajikita kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia matukio mbalimbali yameripotiwa toka Julai hadi Septemba, mwaka huu.

Kwa upande wa Unguja migogoro ya ndoa na talaka (35), huduma za watoto (36), kubaka (46), kulawiti (2), shambulio la aibu (45), kutelekezwa (22), migogoro ya urithi (12), kutorosha (2), kuingiliwa kinyume na maumbile (4) na kukoseshwa haki ya elimu (2).

Kwa upande wake Mwakilishi wa UN Women, Hodan Addou, alisema lengo la kampeni hiyo ni kufikia usawa wa kijinsia kwa sababu wanawake na wasichana wanapitia katika ubaguzi wa usawa na kukabiliwa na vitendo vya udhalilishaji.

Alisema Tanzania imepiga hatua kubwa kwa usawa wa kijinsia na Rais Samia Suluhu Hassan ni mfano bora na kwamba juhudi zaidi zinahitajika ili kuhakikisha kanuni na vikwazo vya kijamii haviendelei kuwawekea kizuizi ushiriki wa wanawake katika siasa na ustawi wa kiuchumi na kuhakikisha kuwa ukatili dhidi ya wanawake na wasichana unakuwa jambo la kawaida.

## Bunge lataka tozo Daraja la Selander

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

BUNGE limependekeza magari yatakayopita katika Daraja Jipya la Selander linalojengwa mkoani Dar es yalipie ushuru kama inavyofanyika katika Daraja la Kigamboni, maarufu kama daraja la Nyerere.

Pendekezo hilo lilitolewa bungeni na Mwenyekiti wa Kamati Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Sillo Baran, wakati akisoma taarifa ya kamati hiyo kuhusu mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2022/23, pamoja na mapendekezo ya mwongozo wa maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/23.

Ujenzi wa daraja hilo lenye urefu wa kilometa 1.03 na upana wa mita 20.5 linatarajiwa kukamilika Desemba, mwaka huu.

Daraja hilo litakapokamilika, litakuwa na barabara unganishi zenye urefu wa kilometa 5.2 na litapita baharini kuanzia ufukwe wa Coco Beach (Oysterbay), kwenda Hospitali ya Aga Khan na linajengwa na Kampuni ya GS Engineering ya Korea.

"Kamati ya Bunge ya Bajeti ilipata fursa ya kutembelea na kukagua ujenzi wa daraja jipya la Tanzanite na kuarifiwa kwamba hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ujenzi wa daraja jipya (kilometa 1.03) na barabara unganishi zenye urefu wa kilometa 5.2 na kwamba ujenzi umefikia asilimia 87.3," alisema Baran.

"Katika kipindi cha mwaka 2020/21, Sh. bilioni 58.8 zimetumika. Kamati inaitaka serikali pindi daraja hili litakapokamilika na kwa sababu limejengwa kwa mkopo kama lilivyo Daraja la Kigamboni liwe ni daraja la kulipia yaani "toll bridge," alisema.

Pasipo kupendekeza gharama ya tozo, Baran alisema kamati imeona kuwa kuna njia mbadala ambayo endapo mtu hataki kulipia, anaweza kupita ni vyema ushauri huo ukazingatiwa. Uzinduzi wa daraja hilo ulifanyika Julai 23, 2018 na Hayati Rais John Magufuli, baada ya serikali kuona tatizo kubwa la msongamano wa magari katika barabara ya Ali Hassan Mwinyi na Barack Obama, Dar es Salaam.

# Vipaumbele vitano bajeti serikali 2022/23

**Na Gwamaka Alipipi,**
DODOMA

SERIKALI imetaja maeneo matano ya kipaumbele yatakayotekelezwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2022/23, ikiwamo kukuza biashara na uwekezaji.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, aliyasema hayo bungeni juzi wakati akiwasilisha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2022/23.

Waziri Mwigulu alisema mpango huo ni wa pili katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano, 2021/22 - 2025/26, wenye dhima ya kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu.

Alisema kwanza, serikali inatarajia kuweka kipaumbele katika kuchochea uchumi shindani na shirikishi ikijumuisha miradi ambayo itajikita katika kujenga jamii yenye uwezo wa kushindana kikanda na kimataifa, kuimarisha utulivu wa uchumi jumla, mazingira ya biashara na uwekezaji.

Pia alisema serikali itajikita katika kuimarisha utafiti na maendeleo pamoja na uhawilishaji wa teknolojia kutoka nje na kuendeleza miundombinu na huduma katika maeneo ya reli, barabara, madaraja, usafiri wa maji, usafiri wa anga, teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), nishati, bandari na viwanja vya ndege

Waziri Mwigulu alitaja kipaumbele cha pili ni kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma. Alisema eneo hilo linajumuisha miradi ya viwanda inayolenga kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na madini pamoja na kuzalisha bidhaa zitakazotumia malighafi na rasilimali zinazopatikana kwa wingi nchini.

"Eneo hili linajumuisha miradi na programu zinazolenga kuboresha sekta ya utalii, huduma za fedha na bima," alisema Waziri Mwigulu.

Alitaja kipaumbele cha tatu ni kukuza biashara na uwekezaji, kwamba eneo hilo linajumuisha programu zitakazoimarisha masoko ya ndani na kutumia fursa za masoko kikanda na kimataifa.

Alisema masoko yanayolengwa ni yale yatakayotoa fursa kwa bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini ikiwamo bidhaa na huduma zitokanazo na kilimo, viwanda na utalii.

Alisema Serikali itaendelea kutekeleza mpango kazi wa kuboresha mazingira ya biashara.

Kipaumbe cha nne, alikitaja ni kuchochea maendeleo ya watu, akifafanua kuwa eneo hilo linajumuisha utekelezaji wa miradi inayolenga kuboresha maisha ya watu ikiwamo kuboresha elimu na mafunzo katika ngazi zote, afya na ustawi wa jamii, hifadhi ya jamii, sensa ya watu na makazi, huduma za maji na mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria hadi jiji la Dodoma.

Aidha, alisema eneo hilo linajumuisha kuimarisha mfumo wa sheria na taasisi za utoaji haki na usimamizi wa utawala bora, ulinzi na usalama na utulivu wa ndani na nje ya nchi, mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi ikiwamo kuimarisha utoaji haki pamoja na ukuzaji wa maadili.

Alisema pia serikali itaendelea na utekelezaji wa shughuli za kuhamishia makao makuu ya Serikali Dodoma ikiwamo awamu ya pili ya ujenzi wa ofisi na miundombinu katika mji wa Serikali Mtumba.

Kipaumbele cha tano ni kuendeleza rasilimali watu, akifafanua kuwa eneo hilo linajumuisha programu na mikakati inayolenga kuendeleza ujuzi wa rasilimali watu nchini, kuanzia ngazi za elimu ya awali hadi elimu ya juu ikiwamo kuwawezesha vijana kujiajiri.



Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na Ofisa Mtendaji Mkuu wa SUMAJKT, Meja Jenerali Rajabu Mabele (wanne kulia), akikata utepe kuzindua zana za kilimo mkakati, magari ya Kampuni ya SUMAJKT Guard Ltd na kampuni ya usafi na unyunyiziaji dawa, Mlalakuwa mkoani Dar es Salaam jana. Kulia kwake ni Mwenyekiti wa Bodi ya SUMAJKT, Meja Jenerali mstaafu Farah Mohamed na (kushoto kwake) ni Mkuu wa Tawi la Utawala JKT na Mwenyekiti wa Kilimo Mkakati, Brigedia Jenerali Hassan Mabena pamoja na maofisa wengine waandamizi. **PICHA: HISANI YA JKT**

# JKT yaongeza vifaa vya kisasa kilimo

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Meja Jenerali Rajabu Mabele, amesema jeshi hilo linaendelea kujiimarisha kwa kuongeza vifaa vingine vya kisasa kuhakikisha mpango wa kilimo mkakati waliouwanzisha unazalisha mara 10 ya mwanzo wakati wakitumia vijana shambani.

Meja Jenerali Mabele aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam wakati akipokea zana za kilimo mkakati, magari ya kampuni ya ulinzi ya SumaJKT na kampuni ya usafi, pikipiki pamoja na kuwekaji wa jiwe la msingi kwa kiwanda cha ubia cha kuzalisha taa za barabarani cha SumaJKT SKYZON kinachogharimu Sh. bilioni 12.896.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Meja Jenerali Mabele alisema JKT imeanzisha kilimo mkakati lengo ikifapo mwaka 2025 wawe na uwezo wa kujitegemea kwa chakula na kuwalisha vijana wanaopata mafunzo ndani ya jeshi hilo.

"Vifaa hivi ni vya kisasa, siku za nyuma tulikuwa tunatumia vijana tulionao wanaingia shambani, sasa hivi tunatumia teknolojia ambapo trekta moja linaweza kufanya kazi ya vijana 1,000 kwa wakati mmoja.

Alisema ununuzi wa magari na pikipiki ni muhimu kwa sababu vitaongeza ufanisi wa utendaji katika kampuni ya usafi na ulinzi walizonazo.

"Kampuni ya usafi na upuliziaji dawa wanafanya kazi zao katika manispaa zilizopo Dar es Salaam na vilevile Dodoma wanasafisha stendi kuu ya mabasi, ili usafi huu ufanyike vizuri na kwa ufasaha lazima tuwe na vifaa, muendelee kuyaenzi mawazo mazuri mliyonayo na mfanye mnayoweza ili kuwezesha shirika kusonga mbele," alisema.

Pia alisema kampuni ya ulinzi ya SumaGuard ina magari na pikipiki na sasa wamekuja na huduma mpya ya magari ya kubeba wagonjwa na kuwataka Watanzania watumie huduma yao.

Kuhusu uwekaji wa jiwe la msingi katika kiwanda cha taa cha SumaJKT SKYZON, alisema mwaka 2018 shirika liliingia makubaliano ya pamoja na Kampuni ya Everlite kutoka Algeria na ujenzi wake ulianza rasmi mwaka 2019 na matarajio yalikuwa ni Julai mwaka huu waanze uzalishaji.

Alisema janga la Uviko-19 lilisababisha nchi nyingi kufunga mipaka yake na mitambo na wataalamu walikuwa wakitokea China hivyo hawakuweza kufanya hivyo kwa wakati uliopangwa.

Alisema Septemba 15, mwaka huu, wataalamu wawili kutoka Algeria ambao wana ubia nao waliwasili Tanzania na kuanza usimikaji wa mitambo na wanatarajia kumaliza kazi hiyo mwezi ujao na kuanza kufundisha wataalamu wa wazawa watakaofanya kazi katika kiwanda hicho kinachoanza kazi mwakani.

Pia taa zinazoagizwa nje ya nchi zitauzwa katika kiwanda hicho kwa bei rafiki kwa Watanzania.

Mkurugenzi wa Tawi la Utawala na Mwenyekiti wa Kilimo Mkakati, Brigedia Jenerali Hassani Mabena, alisema JKT linatekeleza mpango mkakati wa kilimo katika kujulisha na kujitosheleza kwa chakula kwa kutumia zana bora.

Jenerali Mabena alisema JKT limenunua matrekta na zana zake zenye jumla ya Sh. milioni 717.6.

"Kuna kifaa kwa ajili ya kuweka mbegu, vifaa viwili ambavyo vya kuchorea mistari shambani vinatumika kwenye ardhi ngumu, vifaa viwili vya kuwekea mbolea na vifaa vya kuchakata udongo kwenye mashamba ya mpunga," alisema.

Alisema pikipiki na magari ya Suma JKT Guard na ya kupulizia dawa za kuua wadudu yaliyonunuliwa yamegharimu Sh. 393.6.

Vile vile, ununuzi wa magari na pikipiki hizo unafanya kampuni ya ulinzi ya SumaJKT Guard kuwa na magari 48 na pikipiki 111 hadi sasa.

Alisema upande wa kampuni ya usafi na unyunyiziaji dawa wamenunua gari moja ambalo linagharimu Sh. milioni 149.7.

## Sabaya ashindwa tena kufika kortini

**Na Allan Isack,** ARUSHA

HALI ya afya ya aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, imeendelea kuwa tete baada ya kushindwa kufika mahakamani kwa mara nyingine kwa kudaiwa mahakamani kwamba bado ni mgonjwa.

Ole Sabaya na wenzake sita wanakabiliwa na mashtaka matano ya uhujumu uchumi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha.

Washtakiwa wengine ni Silvester Nyegu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31).

Wakili wa Upande wa Utetezi, Mosses Mahuna, jana alidai mahakamani kwamba alipokea taarifa za mshtakiwa huyo kutoka kwa askari Magereza kuwa bado hali yake ya kiafya haijatengemaa.

"Kama tulivyoeleza awali tumepokea taarifa kutoka kwa askari Magereza wakitueleza kuwa hali ya mtuhumiwa sio nzuri bado anaumwa na mimi na mawakili wenzangu, tulipata nafasi ya kwenda kumtembelea na kuonana na daktari wake, na Sabaya alitueleza kwamba endapo atashindwa kufika mahakamani kesi iendelee kusikilizwa," alidai Wakili Mahuna.

Wakili huyo pia alidai kwamba walikwama kuendelea kusikilizwa kwa shauri hilo, labda kama kutakuwapo kwa uamuzi mwingine wa mahakama hiyo .

Naye Wakili wa Serikali Mwandamizi, Othmed Mtenga, alidai kulitakiwa kuwapo mawasiliano ya maandishi kuthibitisha kuwa mshtakiwa huyo, alitoa ridhaa ya kuendelea kusikilizwa kwa kesi hiyo wakati akiwa hayupo mahakamani.

"Kama ulivyokuwa utaratibu tunapendekeza shauri lisiendelee mpaka mawasiliano hayo, kupitia kwa Mkuu wa Gereza yawasilishwe mahakamani kama mshtakiwa ameridhia shauri kuendelea kwa kuwa tunaona kuna umuhimu wa busara kutumia nyaraka kuletwa hapa," alidai.

Wakili Mahuna, alidai kwamba wamesikia ya maombi Jamhuri na hawana kitu cha kuongeza wanatumia fursa hiyo kuomba busara ya mahakama kuwaongoza.

Hakimu Patricia Kisinda, aliahirisha kesi hiyo hadi leo.

"Kutokana na ombi la utetezi kuendelea na kesi kwa kuwa wamepata ruhusa kwa mshtakiwa wa kwanza, mahakama baada ya kupitia ombi hilo, imeona kibali kiwasilishwe kwa njia ya maandishi ili kuweka kumbukumbu kwenye shauri hili," alisema Hakimu Kisinda.

Akizungumza na waandishi wa habari nje ya mahakama, Wakili wa Utetezi, Fauzia Mustapher, alidai kwamba mshtakiwa huyo anasumbuliwa na ugonjwa wa vidonda vya tumbo na alipata akiwa magereza.

Pia alidai kwamba Sabaya, ana tatizo mgongo alililopata ajali wakati anatekeleza majukumu yake akiwa mkuu wa wilaya.

# MATANGAZO

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## OMBI LA KUONESHA NIA KWA AJILI YA UTOAJI WA HUDUMA YA SAMANI ZA OFISI PAMOJA NA UWEKAJI WA SAMANI KATIKA OFISI
## KUMBUKUMBU 0010007217

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V. inaalika taasisi zenye weledi na uzoefu kuonesha nia ya kutoa huduma ya uwekezaji wa vyombo vya ofisini.

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA:**

- EACOP inahitaji huduma kutoka kwa mtoa huduma mwenye uzoefu na sifa nzuri ya kutoa huduma za samani za ofisi pamoja na kuziweka katika ofisi ipasavyo.
- Madawati na meza za kufanyia kazi (vituo vya kazi vinavyoweza kuongezwa na kupunguzwa urefu wakati wa matumizi).
- Meza na viti vya vyumba vya mikutano (kiwango cha kawaida na kiwango cha vyumba vya mikutano).
- Viti vya ofisini vinavyoweza kurefushwa au kufupishwa na vilivyo undwa kwa ajili ya kutoa usaidizi bora kwa mgongo wakati wa kukaa (ergonomic).
- Makabati ya kuhifadhi mafaili (Credenzes).
- Kabati za kuhifadhi vitu mbali mbali.

**VIGEZO MUHIMU:**

Taasisi zitakazoonesha nia zinaalikwa kuambatanisha maombi yao pamoja na taarifa zifuatazo:

- Uthibitisho wa Uzoefu, utendaji, na uwezo katika kutekeleza kazi zilizoainishwa katika mawanda ya kazi, kwa viwango vya juu nchini Tanzania, kwa kufuata viwango vya kitaifa na kimataifa (ikiwa ni pamoja na Viwango vya Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC), na uzoefu wa angalau miaka 5 katika utendaji wa huduma kama hizo ndani ya Tanzania au Kimataifa.
- Uthibitisho wa watendakazi husika wenye vigezo na uzoefu katika uwekaji wa samani katika ofisi.
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa na kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji namsambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia ya kutekeleza shughuli za progamu.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani.
- Uwezo wa kifedha kuweza kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha mahesabu ya fedha ya mwaka 2017.

- Uthibitisho wa sera ya ndani ya Afya, Mazingira na Usalama, taratibu na mchakato kulingana na viwango vya ndani vya viwanda vya kazi husika.
- Uthibitisho wa usajili katika mamlaka husika ndani ya nchi kwa ajili ya utoaji wa huduma husika.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.

---

Taasisi zenye nia ya kuleta maombi na ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu zinapaswa kueleza nia yao kwa lugha ya kiingereza pamoja na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **eacoptz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe 20 Mb) saa au kabla ya saa **11 jinni** za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **….Novemba 2021.** Kichwa cha Habari cha barua pepe kiwe ni kumbukumbu namba husika tu. Kichwa cha Barua Pepe kiwe ni **0010007217.**

---

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia iii kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo iu ndiyo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni. Maelezo yote ya kuonyesha nia yanapaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

21652602

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## OMBI LA KUONESHA NIA YA UTENGENEZAJI, UPIMAJI, USAMBAZAJI NA UTOAJI WA MABOMBA MAKUBWA YA HDPE
## KUMBUKUMBU 0010007214

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V, inaalika taasisi zenye weledi na uzoefu kuonesha nia ya utengenezaji, upimaji, usambazaji na utoaji wa mabomba makubwa ya HDPE Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania, ambapo bomba hilo litapita kwenye mikoa nane (8) ambayo ni Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara, na Tanga; bomba la mafuta pia litapita kwenye Halmashauri za Wilaya 27 na vijiji 231.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA**

EACOP inahitaji huduma za mtengenezaji mwenye uzoefu na mwenye sifa nzuri kutoa huduma za utengenezaji, upimaji, usambazaji na utoaji wa mabomba makubwa ya ukuta wa HDPE kulingana na viwango na vipimo vilivyotajwa hapa chini:

**VIWANGO:**

Ukuta wa muundo wa Bomba za HDPE zitalingana kwa kuzingatia viwango EN 13476-2 / ISO 21138-2, na marekebisho yake, isipokuwa ikiwa imeainishwa vinginevyo.

**VIPIMO:**

- Kuta za kila sehemu ya HDPE (2.45m) zitalingana na vipimo vifuatavyo.
- ID / DN1500 na kipenyo ch nje cha ukubwa 1630 ± 10mm takriban idadi ya mita 400+ zinatakazowasilishwa katika sekesheni za mita 2.45.
- ID / DN1800 na kipenyo cha nje cha ukubwa 1960 ± 10mm takriban idadi ya mita 400+ zinatakazowasilishwa katika sekesheni za mita 2.45.
- KAMPUNI ina haki ya kuthibitisha utengenezaji wa mabomba ya HDPE yaliyowekwa katika kiwanda cha uzalishaji cha Mtengenezaji kulingana na mfumo wa usimamizi wa ubora kulingana na ISO 9001: 2015. Mfumo wa usimamizi wa ubora wa mtengenezaji utahitatakika kuwa uliothibitishwa kwa ISO 9001: 2015 na chombo cha uthibitisho cha Kimataifa.
- Malighafi inayotumika kutengeneza ukuta wa muundo wa bomba za HDPE na viunganishi vyake lazima vilingane na EN13476-1 / ISO 21138-1. Mahitaji ya ubora wa Bomba za HDPE na upimaji wao ni utahitajika kulingana na viwango EN13476-2 / ISO 21138-2, na marekebisho yake husika. Mahitaji ya ubora wa viunganishi zilizotengenezwa kutoka kwa muundo wa bomba za HDPE zitahitajika kulingana na EN 13476-2 / ISO 21138-2, na marekebisho yake ya hivi karibuni.
- Mabomba yote ya HDPE yaliyotengenezwa kwa ukuta yatakayotolewa dhidi ya Zabuni hii "yatatiwa alama" kulingana na viwango vya sahihi vinavyotumika.
- Kwa ombi, nyaraka za ubora wa bidhaa zinazotolewa zinapaswa kuwasilishwa na mtengenezaji kupitia vyeti vya kufanya kazi kulingana na viwango vinavyotumika. Rekodi zote za matokeo ya vipimo vya ubora zitahifadhiwa na mtengenezaji kwa marejeleo yajayo.

- Kabla na baada ya kutoa zabuni kwa Mtengenezaji, KAMPUNI ina haki ya kukagua uwezo wa upimaji na kushuhudia majaribio yaliyofanywa katika kituo cha Maabara cha Mtengenezaji kutathmini ubora wa bidhaa kulingana na viwango vinavyotumika. KAMPUNI itateua mwakilishi kushuhudia majaribio yote yaliyofanywa katika kituo cha maabara cha Mtengenezaji na mwakilishi atawasilisha matokeo yote ya mkandarasi/mzabuni husika & KAMPUNI kwa kujitegemea. KAMPUNI ina haki ya kuidhinisha Bidhaa kulingana na ripoti za majaribio ya ubora kabla ya kupelekwa kwenye eneo la ujenzi.

**VIGEZO MUHIMU VYA KUZINGATIA**

Taasisi zitakazoonesha nia zinaalikwa kuambatanisha maombi yao pamoja na taarifa zifuatazo:

- Uzoefu, utendaji, na uwezo katika kutekeleza kazi zilizoainishwa chini ya upeo wa kazi, kwa kiwango kikubwa nchini Tanzania, kwa kufuata viwango vya kitaifa na kimataifa (ikiwa ni pamoja na Viwango vya Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC), na uzoefu wa angalau miaka 15 katika utendaji wa huduma kama hizo ndani ya Tanzania au Kimataifa.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.
- Maelezo mafupi kuhusu uzoefu na uwezo wa:

  Utekelezaji wa programu za aina hiyo kwa viwango vya fedha vya kimataifa kwa ajili ya miradi mikubwa yo miundombinu nchini Tanzania.
- Kusimamia miradi mikubwa na wakandarasi washirika.
- Kufanya kazi kwa kushirikiana na serikali za mitaa na sekta binafsi.
- Wafanyakazi waliopendekezwa kufanya kazi kwenye Mradi huu na ujuzi na uzoefu wao katika kutekeleza programu za aina hii.
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa na kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia ya kutekeleza shughuli za progamu.

---

Mawanda haya yanaweza kugawanywa kimkoa au kiutalaam na KAMPUNI inaruhusu Wazabuni kuwasilisha pendekezo kwa ajili ya kipengele kimoja, kadhaa au vyote.

Taasisi zenye nia na ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu zinapaswa kuwasilisha nia kwa lugha ya kiingereza pamoja na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe 20 Mb) saa au kabla ya saa **11 jioni** za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **09 Novemba 2021.**Kichwa cha Habari cha Barua Pepe kiwe ni **0010007214.**

---

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia ili kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo tu ndiyo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni. Maelezo yote ya kuonyesha nia yanapaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

21653602

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Miradi 43 ya kimkakati iwanufaishe wananchi

**KITUO** cha Uwekezaji Tanzania (TIC), kimesajili miradi mikubwa ya kimkakati kwa kupewa hadhi ya miradi mahiri ipatayo 43, ambayo itatoa ajira kwa Watanzania 130,720.

Aidha, serikali inasema miradi hiyo inatarajia kuwekeza kiasi cha Dola za Marekani 12,278, na manufaa makubwa yanatarajiwa kuonekana kwa mwananchi mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji, Geofrey Mwambe, akizungumzia miaka 60 ya Uhuru, alisema miradi hiyo inahusisha sekta mbalimbali za uzalishaji viwandani, majengo ya biashara, ujenzi na madini.

Hizi ni habari njema kwa Watanzania wengi kwa kuwa sasa miradi hiyo inakwenda kusukuma maendeleo yao, na zaidi ajira kwa wenye sifa ya kuajiriwa moja kwa moja na wengine sio moja kwa moja.

Miradi 43 ikisambaa maeneo mbalimbali nchini ni wazi kuwa kuna manufaa ya moja kwa moja na yasiyo ya moja kwa moja kwa mtu binafsi na taifa kwa ujumla.

Pia, kuna habari njema ya ajira ambayo ni kilio cha watu wengi kwa sasa ambao wamesoma vizuri hadi ngazi ya shahada ya kwanza na ya pili, lakini hawajapata ajira kwa kuwa hazipo.

Lakini kampuni zitakazowekeza kwenye maeneo hayo zitatekeleza sheria ya uwajibikaji kwa jamii kwa miradi inayoibuliwa na jamii husika, ili kuendelea kujenga uhusiano mwema baina yao.

Chini ya utaratibu huo, mwekezaji anakaa na jamii kupitia kamati zao ambazo hujadili nini cha kusaidia hasa kwa kuangalia uhitaji wao na uwezo wa mwekezaji kwa kile alichotenga cha kusaidia.

Kuna umuhimu kampuni au wawekezaji wakatilia mkazo katika hili ili tuone miradi yenye kubadilisha maisha ya wananchi husika, kuliko kuwa na miradi ya d'anganya toto' ambayo siyo endelevu na haina manufaa kwa Watanzania.

Tuna mifano mingi ya maeneo yenye rasilimali ambayo wananchi wake ni fukara kiasi kwamba utajiri uliopo kwenye eneo lao hauwanufaishi kwa namna yoyote ile na linapokuja suala la ajira wanaishia katika ajira za ndogo ambazo haziwaingizii kipato cha kutosheleza mahitaji ya msingi.

Ni muhimu ajira zinazotajwa ziwe na ajira nzuri na zisihesabike ajira za muda mfupi yaani vibarua ambao hulipwa wastani wa Sh. 3,000 hadi 5,000 kwa siku, kiasi ambacho hakimwezeshi mtu kumudu mahitaji ya msingi.

Matarajio ya wananchi wanaposikia neema ya ajira ni kwa watu wetu waliosoma vyema na wako mtaani bila ajira, na isiwe ni kuja kuwa vibarua wakati ajira nzuri wanapewa wageni.

Ni muhimu kuwatazama wananchi wasio na ajira, wanaotaabika kwa maisha magumu ndio waingie mikataba minono na wawekezaji ambao mwisho wa siku wanaweza kuondoka na kuacha athari za muda mrefu kwenye maeneo ya jamii.

Mathalani, maeneo ya migodi unakuta wananchi ni fukara, lakini mali inayotoka ardhini ni ya thamani kubwa, lakini hawana huduma muhimu za kijamii kama zahanati, vituo vya afya na hospitali, kitu ambcho hakikubaliki.

Ni lazima kujifunza kutokana na haya kwamba kila mradi unaokuja mbali na kuwa na manufaa kwa mwekezaji, lakini manufaa kwa mwananchi mmoja mmoja na jamii husika yaonekane.

Kuna mifano ya nchi kama Nigeria yenye utajiri wa mafuta katika eneo la Delta, lakini hadi leo ndilo eneo lenye watu maskini kupindukia. Haitapendeza kurekodi miradi mingi ambayo kimsingi inashindwa kuonyesha mabadiliko kwenye maisha ya mwananchi mmoja mmoja.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Tushikamane na Rais Samia kwa alichoanza nacho, kazi iendelee!

Na Anthony Gervas, Mwanza

**'KAZI** Iendelee' ni kaulimbiu ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, ikichukua nafasi ya ndugu yake wa awamu iliyotangulia ya tano "Hapa Kazi Tu.

Kaulimbiu hiyo ya sasa ina maana kubwa kwa Watanzania katika utekelezaji miradi mbalimbali ya maendeleo iliyoachwa na mtangulizi wake Hayati Dk. John Magufuli, aliyeongoza nchi kwa miaka mitano.

Lakini, Watanzania wenzangu kile kilichofanyika kwenye Awamu ya Tano, kila mtu alikiona na kusikia! Huhitaji kuambiwa wala kusimuliwa.

Sasa, kaulimbiu ya Rais Samia Suluhu Hassan, ni mwendelezo wa utekelezaji miradi ya maendeleo ya wananchi ambayo haijakamilika na kuanzisha miradi mipya.

Baada ya Rais Samia kupokea kijiti kutoka kwa mtangulizi wake, amewaahidi Watanzania kuhakikisha miradi yote inakamilika ikiwamo ya barabara na kufua umeme wa Bwawa la Mwalimu Nyerere na mingine katika sekta za Elimu, Afya na Maji.

Leo mimi nazungumzia kaulimbiu ya serikali ya Awamu ya Sita, wengi tukiwa na imani kubwa na mama yetu Rais Samia kwamba ataisimamia miradi hiyo kikamilifu. Hapo umo ujenzi wa mradi wa Stendi ya Mabasi Magufuli, eneo la Mbezi jijini Dar-es Salaam ambao bado haujakamilika vizuri

Mradi huo ni mkubwa utakaoingiza mamilioni ya shilingi kutokana na kodi mbalimbali za Watanzania na watumiaji wengineo, wakiwamo wananchi wanaosafiri kila siku kutoka ndani ya jiji hilo kwenda mikoani mbalimali, pia wanaoingia.

Tanzania ina jambo la kujivunia kuwa na miradi mingi kama hiyo. Huo bado haujakamilika kujengwa katika sehemu mbalimbali, ikiwamo soko la mama lishe ambalo miundombinu yake kwa sasa siyo rafiki hasa, kwa kutoa huduma za chakula. Soko hilo ni fursa kubwa na ajira tosha kwa waliyoipata nafasi kutia huduma lishe.

Hivi sasa mamalishe wanatoa huduma ya chakula kwenye vibanda vyao ambavyo havina sakafu, vina vumbi. Pia, wanafanya biashara katika mazingira hatarishi kiafya hasa nyakati hizi za mvua, kunaweza kutokea mlipuko wa magonjwa kama kipindupindu.

Mamlaka husika zinatakiwa kusaidia kuboresha miundombinu katika soko hilo, ikiwamo mitaro na mifereji ya maji, kilichobaki kwa serikali ni kumalizia ujenzi huo ambao uko katika hatua nzuri za mwisho.

Lakini naamini, serikali ya Mama wetu msikivu anayekwenda pamoja na Watanzania, itakamilisha ahadi zake za kukamilisha miradi yote iliyopo na kuanzisha mipya, naamini tutasonga mbele daima katika duru za maendeleo.

Rais Samia alipoingia madarakani, aliwatahadhalisha watendaji serikalini kuwa wachape kazi na siyo kuonea wananchi wa chini. Altamka, macho yake yanaona mbali na 'mtu akimzengua watazenguana' bila kuangalia cheo cha mtu wala sura, itikadi za kisiasa, dini au kabila.

Watanzania tunaamini atasimama imara kama anavyoendelea kufanya sasa. Kiongozi atakayekwenda kinyume na utaratibu wa serikali yake hata kama alimteua yeye atamtengua bila kuogopa. Hata sisi watu wa chini tuko pamoja naye.

Siasa na sera za uongozi ndizo zinazosababisha kukwama maendeleo. Watanzania tuzipuuze, wagombea wa nafasi mbalimbali za uchaguzi wanapoenda kwenye kampeni zao, wapo ambao huwajaza maneno mazuri wananchi yasiyokuwa na utekelezaji wa kile walichokiahidi, pindi wanapokalia madaraka yao.

Wananchi kudanganywa kwa chumvi na sukari na kupiga kura kwa mtu muongo ni mambo yaliyopitwa na wakati, mtu anapopata uongozi anakuwa hakumbuki tena shida za umma. Mara zote kiongozi wa aina hiyo tuwanyimeni kura, ili wajifunze hata wengine.

Nirejee nikisema, Rais wetu Samia ndiye Amiri Jeshi Mkuu nchini, tunayemtegemea kwa kila jambo, hivyo asisite pale anapoona kiongozi au mtendaji akifuja fedha za serikali. Amchukulie hatua, pasipo kujali nafasi yake ili 'Kazi Iendelee!'

## HABARI PICHANI

# ZIARA YA BALOZI WA INDIA NCHINI SHRI BINAYA SRIKANTA PRADHAN KATIKA VYOMBO VYA HABARI VYA IPP




Balozi wa India nchini, Shri Binaya Srikanta Pradhan (kulia), akipata maelezo kutoka kwa Mhariri Mtendaji wa gazeti la The Guardian, Wallace Maugo (watatu kulia), alipotembelea chumba cha habari cha Kampuni ya The Guardian Ltd (TGL) inayochapisha magazeti ya The Guardian na Nipashe, Mikocheni, mkoani Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mhariri Mtendaji wa gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe na (watatu kushoto) ni Mkurugenzi wa TGL, Joyce Luhanga.



Meneja wa kiwanda cha uchapishaji cha TGL, Balasubramaniyan Venkadachalam (kulia), akitoa maelezo kwa Balozi Shri Binaya Srikanta Pradhan (kushoto), kuhusu uchapishaji wa magazeti.

**PICHA ZOTE: MIRAJI MSALA**



Balozi Shri Binaya Srikanta Pradhan (kulia), akimsikiliza Meneja wa EATV na Radio, Lydia Igarabuza alipotembelea studio. Watatu kulia ni Mkurugenzi wa Ubalozi wa India, Santhopsh G R.



Balozi Shri Binaya Srikanta Pradhan (wapili kulia), akimsikiliza Mtangazaji wa Redio One, Othuman Suleyman, alipotembelea studio za redio hiyo.



Mkurugenzi Mtendaji wa ITV/Radio One, Joyce Mhavile (kulia), akitoa maelezo kwa Balozi Shri Binaya Srikanta Pradhan (wapili kushoto) alipoitembelea kampuni hiyo.



Mkurugenzi wa Vipindi wa ITV, Pius Paul (kushoto), akitoa maelezo kwa Balozi Shri Binaya Srikanta Pradhan, jinsi taarifa ya habari inavyorushwa ndani ya studio ya televisheni hiyo.

# Wananchi Jangwani wamwangukia waziri

Na Munir Shemweta

BAADHI ya wakazi wa Jangwani jijini Dar es Salaam, wamemwomba Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Mkazi, Dk. Angeline Mabula, kusaidia mwekezaji kupewa eneo hilo ili wapate fidia.

Wakazi hao waliwasilisha ombi hilo jana wakati Dk. Mabula alipotembelea Jangwani kujionea mazingira kama ni salama kwa uwekezaji sambamba na mipango ya mamlaka husika kuhusu eneo hilo.

Kampuni ya Jangwani Holding Ltd imeomba kuwekeza sehemu katika eneo la Jangwani na kukubali kuwalipa fidia wakazi wake. Hata hivyo, uamuzi wa kutoa eneo hilo kwa ajili ya uwekezaji unasubiri ushirikishwaji wa mamlaka husika ambazo ni Ofisi ya Makamu wa Rais Idara ya Mazingira, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam (Ilala) pamoja na Mradi wa Uendelezaji Jiji la Dar es Salaam (DMDP).

Wakizungumza katika eneo hilo juzi, wakazi hao walisema wanachohitaji kwa sasa ni mwekezaji kupatiwa sehemu ya eneo la Bonde la Jangwani ili nao walipwe fidia na kwenda kutafuta maeneo mengine ya kuishi.

Kwa mujibu wa wakazi hao, eneo hilo limekuwa na changamoto ya mafuriko kwa muda mrefu na juhudi za awali za serikali kuwapatia maeneo wananchi Mabwepande Wilaya ya Kinondoni halikidhi wakazi wote kwa kuwa walipatiwa viwanja walikuwa 43 kati ya 1,200.

"Imekuja kampuni inataka kutuhamisha hapa na itulipe fidia, lakini mamlaka husika hazijaridhia huku halmashauri ya jiji ikishindwa hata kuweka vibao kuonyesha kuwa eneo hili ni hatarishi na maeneo yamewekwa vifusi na kuendelea na shughuli kama kawaida," alisema mwananchi mmoja. Kwa sasa, walisema wako hoi bila ya kujua hatima yao na kuomba mwekezaji kupewa eneo ili waondoke kwenda kutafuta sehemu zingine za kuishi kwa kuwa baadhi ya nyumba zao zimeharibika.

Salehe Cheyo, aliyejitambulisha kama Mjumbe wa Mtaa wa Msimbazi Bondeni, alisema kiu kubwa ya wakazi wa eneo la Jangwani ni kuona mwekezaji anapatiwa eneo hilo ili walipwe fidia na kudai kuwa kinachowashangaza ni kuelezwa eneo hilo ni hatarishi wakati limekuwa likipatiwa huduma mbalimbali kama vile maji na umeme na wananchi wamekuwa wakilipia huduma hizo.

Naibu Waziri Mabula aliwaomba wakazi wa eneo hilo kuwa na subira wakati serikali ikilifanyia kazi suala hilo kwa kuwa kuna mamlaka na mipango tofauti na kwamba serikali lazima ijiridhishe kama uwekezaji hautakuwa na madhara sambamba mipango ya uendelezaji.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, kabla ya uamuzi kufanyika lazima baadhi ya mamlaka zishirikishwe ili uamuzi utakaotolewa uwe na tija na mamlaka hizo.

"Mambo yakienda vizuri watawekeza lazima mvute subira na kilichonileta hapa ni kujiridhisha eneo ni salama? Je, liko katika mpango gani na wahusika wamejiridhisha? Hatuwezi kupitisha leo halafu kesho kunatokea maafa. Naomba muwe na subira" alisema.



Meya wa Jiji la Zanzibar, Mohamoud Mohamed Mussa (watatu kulia), akikabidhi kikombe kwa mwanafunzi wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Mtopepo B, Khalid Mohamed Said, baada ya kuibuka mshindi wa shindano la mchoro wa usalama barabarani kwa shule za msingi Zanzibar lililoandaliwa na Kampuni ya mafuta ya Puma Tanzania kwa kushirikiana na Amend, jijini humo jana. Wengine ni viongozi kutoka kampuni ya Puma, Amend na walimu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wanahabari wapewa tano hamasa corona

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

IDARA ya Afya mkoani Rukwa, imewapongeza na kuwashukuru waandishi wa habari mkoani humo kushiriki katika kuhamasisha wananchi.

Kwamba kitendo hicho kilisababisha mkoa huo kufikia lengo la utoaji wa chango ya kujikinga na ugonjwa wa Uviko 19 kwa asilimia 100.

Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Ally Lubeba, aliyasema hayo wakati akifungua mafunzo ya siku moja kwa waandishi wa habari yaliyoandaliwa na Idara hiyo kwa lengo la kuwajengea uwezo wanapokuwa katika jukumu la kuwahamasisha wananchi kupata chanjo ya Uviko -19.

Alisema kuwa waandishi wa habari kupitia vyombo vyao hasa vilivyomo mkoani humo, wamefanya kazi kubwa ya kuwahamasisha wananchi kupata chanzo na kufanikisha kufikia lengo la asilimia 100 kwa awamu ya kwanza.

"Tuna kila sababu ya kuwapongeza na kuwashukuru wanahabari kwa kazi mkubwa mliyoifanya ya kuwahamasisha wananchi wajitokeze kupata chanzo, kitendo kilichosaidia kufikia lengo kwa asilimia mia moja," alisema

Alisema hivi sasa Mkoa wa Rukwa umepata awamu ya pili chanjo aina ya Sinopharm dozi 24,183 ambazo zimeanza kutolewa katika vituo vilivyotengwa kwa ajili ya utoaji chanjo hiyo.

Aliwaomba wanahabari hao kuendelea na kazi ya kuwahamasisha wananchi kujitokeza kupata chanjo hiyo kwani chanjo zipo nyingi na zinatolewa bure na serikali hivyo ni muhimu kwao kuchanja ili wajikinge wao pamoja na familia zao.

# Kampuni Tanzania zasota ushiriki usindikaji mazao

Na Mwandishi Wetu

USHIRIKI wa kampuni ndogo kwenye usindikaji wa mazao ya kilimo uko chini nchini Tanzania na Afrika Kusini, utafiti umebaini.

Afrika Kusini kampuni kubwa chache zinahodhi soko la usindikaji na kuacha nafasi ndogo kwa kampuni ndogo wakati Tanzania ushiriki wa wasindikaji wadogo unakwazwa na mfumo hasi wa soko, mtaji mdogo na ushirikiano haba na wadau.

Utafiti huo uliofanywa kwenye nchi mbili zinazotofautiana kiuchumi, umetazama usindikaji wa mahindi, maziwa na matunda jamii ya machungwa na kubaini kuwa ushiriki wa wawekezaji wadogo kwenye usindikaji mazao umedumazwa na mifumo hodhi ya kibiashara na ukosefu wa sera rafiki.

utafiti huo uliofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Kiuchumi na Kijamii nchini Tanzania (ESRF) na vyuo vikuu vya Johannesburg na Edinburgh, umefadhiliwa na Baraza la Utafiti wa Kiuchumi na Kijamii la Uingereza (ESRC).

Pia, umebaini ushiriki wa kampuni ndogo katika usagishaji mahindi Tanzania ni asilimia 90 ya mzigo wote. Wakati huo huo, ni asilimia 14 pekee ya lita bilioni 2.5 za maziwa zinazozalishwa Tanzania kwa mwaka zinazosindikwa na kampuni ndogo takribani 80 zenye uwezo wa chini ya lita 5,000 kwa siku.

"Kuna kampuni kubwa tatu zinazoweza kusindika hadi lita 50,000 kwa siku kila moja. Sehemu kubwa ya maziwa yanayozalishwa huuzwa moja kwa moja majumbani kupitia wachuuzi na mawakala," utafiti umebaini.

Pia, utafiti huo umebaini kutokuwapo kwa usindikaji wa matunda jamii ya machungwa kwa sababu matunda hayo yanayolimwa mikoa mitatu ya Tanzania ni ya aina mbali mbali yenye kiwango cha chini cha sukari kisichofaa kwa utengenezaji wa juisi.

"Kampuni kubwa zinazotawala biashara ya maziwa zinashutumiwa kwa kukiuka maadili na kutumia vibaya nguvu yao ya kifedha kukandamiza kampuni ndogo sokoni."

Utafiti ulibaini pia kuwa maduka makubwa ya vyakula yanayouza sehemu kubwa ya bidhaa za maziwa, yanaweka masharti ya uonevu dhidi ya kampuni ndogo.

Kadhalika utafiti umebaini Tanzania uzalishaji na usindikaji wa machungwa na jamii yake ni biashara kubwa Afrika Kusini, ambayo ni ya pili duniani kwa kuuza nje bidhaa hiyo.

Utafiti umebainisha kuwa wasindikaji wadogo wa mahindi Tanzania wanatumia mashine duni kwa kukosa uwezo wa kuboresha teknolojia, wakati kampuni kubwa zinatumia mitambo mikubwa kuzalisha idadi kubwa ya bidhaa zenye chapa ya wazalishaji kwa gharama nafuu.

Watafiti wanasema kuna hatua za kisera zilizochukuliwa kuhusiana na zao la mahindi nchini Tanzania, lakini juhudi hizo zililenga upande wa uzalishaji tu bila kuangalia ushiriki wa kampuni ndogo kwenye usindikaji wa zao hilo.

Hakuna hatua iliyochukuliwa kunusuru zao la machungwa ambalo limeachwa bila huduma ya utafiti na msaada wa elimu kwa wakulima. Uzalishaji wa maziwa pia umeonekana kutotiliwa mkazo wa kutosha, ukiachiwa wafugaji wa ng'ombe wa kienyeji. Nchi ina asilimia tatu pekee ya ng'ombe wa maziwa wa kisasa.

Taarifa ya utafiti inashauri Serikali za Tanzania na Afrika Kusini kuchukua hatua madhubuti kuwezesha kampuni ndogo zijiimarishe kiteknolojia na kifedha ili zihimili ushindani katika biashara ya usindikaji mazao ya kilimo. Benki imara za maendeleo zianzishwe kutoa mikopo kwa kampuni ndogo Tanzania.

Hata hivyo, watafiti wametahadharisha kuwa Afrika Kusini ina mazingira ya kipekee wakulima wa machungwa wana chama imara na hutumia nguvu ya umoja wao katika majadiliano na wadau wa biashara kupata maslahi bora.

Utafiti huo linganishi umeangazia mambo yanayochangia ubunifu na ushirikishwaji kwenye usindikaji wa mazao ya kilimo, changamoto zinazokabili kampuni ndogo katika sekta hiyo na jinsi ya kutumia matokeo ya utafiti kusaidia utengenezaji wa sera za kilimo kitaifa na kikanda.

Matokeo ya utafiti huo yaliwasilishwa kwenye mkutano wa mtandaoni mwishoni mwa Agosti mwaka huu na kujadiliwa na wataalamu kutoka vyuo vikuu mbali mbali.

# Sababu mwenyekiti kutishia kung'atuka

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Ngassa Mboje, ametishia kujiuzulu nyadhifa hiyo, kwa madai ya kutoheshimiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Nice Munissy.

Mboje alisema hayo kwenye kikao cha Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, baada ya kumaliza kukagua maendeleo ya ujenzi wa Kituo cha Afya Salawe, na madarasa matatu katika Shule mpya ya Sekondari Mhangu iliyopo Salawe.

Alisema kwenye Halmashauri hiyo tangu aingie Mkurugenzi huyo mpya hakuna tena kuheshimiana wala maelewano mazuri, hivyo kuona ni bora aachie ngazi ya uenyekiti ili abaki kuwatumia wananchi wake wa Kata ya Mwalukwa.

"Tangu 2011 nipo kwenye Halmashauri hii, na wakurugenzi wote waliopita walikuwa wakiniheshimu, lakini sasa hivi hakuna heshima, ni bora nikachukua uamuzi wa kuachia ngazi ya uenyekiti nibaki na udiwani wangu kutumikia wananchi," alisema Mboje.

" Kwenye Halmashauri hii naona kuna changamoto kubwa inakuja kutokea, watumishi hawazunguzi tu kuna shida kubwa sana," aliongeza.

Aidha, katika ziara ya Mkuu huyo wa Mkoa wakati wa kutembelea miradi ya maendeleo, Mwenyekiti huyo alikuwa akilalamika kuwa amenyimwa gari na mkurugenzi, kwa sababu ya kutomheshimu, hivyo kulazimika kupanda kwenye gari la Chama cha Mapinduzi (CCM).

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo Nice Munissy, akizungumzia suala la magari, alisema Halmashauri hiyo ina magari 24, lakini sita ndiyo yanafanya kazi na yaliyosalia yote ni mabovu.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Sophia Mjema, alimtaka Mboje asiwe mnyonge, bali kama kuna upungufu amwite Mkurugenzi wakae wamalize changamoto zao.

Pia, alisema kama haiwezekani amwite kwenye kamati ya siasa ya CCM ,ili wasuluhishwe, kwa sababu kama Mwenyekiti na Mkurugenzi hawana maelewano mazuri, Halmashauri hiyo haiwezi kusongambele kimaendeleo.

# Taasisi yaja na suluhisho tatizo la utapiamlo

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA bado inakabiliwa na tatizo kubwa la udumavu unaosababishwa na utapiamlo kutokana na kula vyakula vyenye lishe duni.

Hadi kufikia Juni 2021, asilimia 31.8 ya watoto chini ya miaka mitano Tanzania, walikuwa na tatizo la udumavu unaosababishwa na utapiamlo sugu kutokana na kula vyakula vyenye lishe duni na visivyo na virutubisho vya kutosha na kusababisha udumavu kwa watoto wachanga kushindwa kukua ipasavyo.

Suluhisho pekee la tatizo hili ni matumizi ya teknolojia ya kisasa ya kibailojia ya kuzalisha mbegu zenye viini lishe iitwayo, Bayofotifikesheni (Biofortification), hivyo umetolewa wito kwa wazalishaji, wasindikaji na wauzaji vyakula wa sekta ya umma na sekta binafsi kuchukua hatua madhubuti kuboresha mifumo ya uzalishaji chakula ya Tanzania tuzalishe vyakula vyenye lishe bora ili kukabiliana na tatizo la udumavu unaosababishwa na utapiamlo.

Wito huo ulitolewa na Afisa Programu kutoka taasisi ya GAIN Tanzania, Mariam Luhambati kwenye ofisi za Global Alliance for Improved Nutrition (GAIN), jijini Dar es Salaam, wakati wa maonyesho ya maalum ya technolojia za uboreshaji chakula duniani, unaofanywa na GAIN na wadau wake.

Alisema kwa vile mahindi na maharagwe ndio chakula kikuu cha Watanzania wengi, taifa likifanikiwa kuhakikisha mahindi na maharage yote yanayolimwa nchini, yawe yenye viini lishe hivyo kila Mtanzania, na haswa vijijini, watapata mlo bora wenye lishe bora na kumaliza kabisa tatizo la udumavu na utapiamlo nchini.

Luhambati alisema njia ya kufanikisha zoezi hili, ni kwa serikali kusisitiza mbegu zote za mahindi na maharagwe zitakazosambazwa nchini Tanzania kwa wakulima wote, lazima ziwe ni mbegu ziliiongezwa viini lishe kwa kutumia utaalamu wa kisasa wa utengenezaji wa mbegu uitwao Biofortification ambapo mbegu zenye viini lishe, zinapandwa pamoja na mbegu za kawaida, hivyo zinaota pamoja, na kupitia tekinolojia ya kibaiyolojia, vile viini lishe kutoka mbegu zenye viini lishe, zinaambukiza zile mbegu nyingine zisizo na viini lishe, hivyo mazao yote yanayoota yanakuwa na viini lishe.

Alisema Biofortification ni utaalamu wa kuongeza viini lishe vya vitamini na madini katika mazao kwa kutumia utaalanu wa kibayolojia, ambapo taasisi ya GAIN kwa ushirikiano na taasisi ya HarvestPlus zinafanya kazi na wadau mbalimbali kupitia Mpango wa Kufanya Biashara ya Mazao Yanayorutubishwa (CBC) ili kuendeleza na kukuza aina za vyakula vikuu vilivyorutubishwa na virutubishi ambavyo kwa kawaida huzalishwa kwa viwango vya juu vya madini ya chuma, zinki au vitamini A, ambavyo vinahitajika kwa ajili ya kudumisha afya bora na maendeleo ya binadamu.

Kwa Tanzania, Mpango huo unaangazia mazao makuu mawili ambayo ni mahindi yenye vitamini A na maharagwe yenye madini ya chuma.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema (kulia), akishiriki kufyatua tofali kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa katika Shule ya Sekondari Solwa wilayani Shinyanga jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Nice Munissy. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Wakulima kukopeshwa mabilioni kwa riba nafuu

**Na Mwandishi Wetu**

WAKULIMA wadogo wametangaziwa neema, baada ya Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kuingia katika makubaliano na Maendeleo Benki kuwawezesha kupata mikopo yenye riba nafuu.

Lengo ni kuwawezesha kuongeza uzalishaji na kufanya mageuzi katika sekta ya kilimo, uvuvi na ufugaji.

Makubaliano hayo, yaliyosainiwa katika makao makuu ya TADB jijini Dar es Salaam, yataiwezesha benki hiyo kutoa dhamana ya Sh. bilioni mbili kwa wakulima watakaokwenda kuomba mikopo Maendeleo Benki kufanya shughuli za kilimo, ufugaji pamoja na uvuvi kwa riba nafuu ya asilimia isiyozidi 15. Dhamana hii inaratibiwa na TADB chini ya mfuko maalum wa dhamana kwa wakulima wadogo nchini 'SCGS'.

"TADB inaendeleza dhamira yake ya kuwezesha upatikanaji wa mitaji kwa wakulima wadogo na wa kati. Wakulima wetu nchini wanapata changamoto ya mitaji. Wengi wakilazimika kukopa kwa riba za kibiashara ambapo wengi wao wamekuwa wakipata changamoto ya kuhimili riba hizo kubwa. Hivyo, kama taasisi ya maendeleo ya kifedha, kupitia mfuko wa dhamana kwa wakulima wadogo, tumeona umuhimu wa kutoa mikopo hii nafuu kwa kushirikiana na Maendeleo Bank ili kuwawezesha wakulima wengi zaidi kupata mitaji," alieleza Derick Lugemala, Mkurugenzi wa TADB.

Kwa upande wake mkuu wa kitengo cha biashara wa Benki ya Maendeleo, Emmanuel Mwaya, alisema mikopo hiyo watakayokuwa wanatoa kwa dhamana ya TADB itawawezesha kuwakopesha wakulima wadogo mikopo ya mtaji hadi kiwango cha Sh. milioni 50 kwa mkulima mmoja mmoja, Sh. Milioni 500 milioni kwa vikundi na vyama vya wakulima, na hadi Sh.bilioni 1 kwa kampuni ambazo miradi yake inawaunganisha na kuwanufaisha wakulima wadogo wengi.

"Ili kupata mikopo hii, mkulima anahitaji kufika katika tawi letu lolote kwa kuwa mikopo hii inapatikana katika matawi yetu yote. Tunatoa rai kwa wakulima wote wadogo kuchangamkia fursa hii."

Awali, Lugemala alisema lengo la mikopo hiyo yenye masharti nafuu ni kuchagiza benki za kibiashara na taasisi za kifedha kutoa mikopo zaidi kwa wakulima na kuwezesha ukuaji wa minyororo yote ya thamani yanayohusiana na kilimo, uvuvi na ufugaji nchini.

"Mpaka Desemba 2020, mfuko huu wa dhamana ulikwisha toa mikopo katika miradi ya kilimo, uvuvi na ufugaji yenye thamani ya Sh. bilioni 106 na kuwafikia wanufaikaji zaidi ya 11,000 moja kwa moja na wasionufaika moja kwa moja 750,000. Baadhi ya miradi tuliyowezesha ni pamoja na mnyororo wa thamani wa mazao ya korosho, mpunga, kahawa, miwa, mahindi, mihogo, pamba na ufugaji wa kuku," alifafanua Lugemala.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka TADB, mfuko huu wa dhamana ulianzishwa Februari 2018. Na katika kipindi cha miaka mitatu sasa, TADB imeshashirikiana na benki na taasisi za kifedha kama NMB, CRDB, Azania, Benki ya Posta (TPB), Stanbic, FINCA Microfinance, UCHUMI Commercial Bank, Tandahimba Community Bank (TACOBA), Mufindi Community Bank (MUCOBA), NBC na Maendeleo Bank.

"TADB inaamini kwamba kupitia mtandao huu wa ushirikiano wa kimkakati, idadi kubwa ya wakulima wadogo watafikiwa na kuwezeshwa," alisisitiza Lugemala.

# Mipakani sasa kupata mawasiliano ya uhakika

SERIKALI imejipanga kupeleka mawasiliano ya uhakika katika maeneo ya mipakani kutokana na masuala ya kiusalama.

Naibu Waziri wa Habari, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Mhandisi Andrea Kundo, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota.

Katika swali lake, Chikota alihoji mkakati wa serikali wa kufikisha mawasiliano katika kata zilizopo mpakani na Msumbiji kutokana na kuwepo na tatizo la kiusalama.

"Serikali ina mpango gani kuhakikisha kata hizi kwasasa zinakuwa na mawasiliano ya uhakika naomba mpango wa haraka wa serikali,"alisema.

Hata hivyo, alisema minara ya simu inayojengwa kwasasa ni kwa ajili ya mawasiliano ya kupiga na kupokea simu na sio intaneti.

"Kuna mahitaji makubwa ya intaneti vijijini kwasasa na hata ilani yetu ya CCM inadhamiria kuboresha upatikanaji wa intaneti vijijini sasa serikali ina mpango gani wa kuboresha minara ili intaneti ipatikane vijijini?"alihoji. Akijibu maswali hayo, Kundo alisema walishafikia kwenye maeneo hayo na serikali imepanga kutekeleza kupitia miradi ya mipakani.

"Mbunge asiwe na wasiwasi kabisa serikali kupitia dhamira yake ile ile itahakikisha Watanzania wanapata mawasiliano,"alisema.

Kuhusu intaneti, alisema hadi sasa serikali inaboresha miundombinu ya mkongo wa taifa.

"Kwa upande wa kusini ukitoka pale Mangaka kwenda Mtambaswala takribani kilometa 72 tunajenga mkongo wa taifa na siku za hivi karibuni mradi utakamilika,"alisema.

Aidha, alisema serikali ilishaagiza watoa huduma wote kuhakikisha miradi yote itakayojengwa kuanzia sasa iwe inatoa huduma ya intaneti kwa kiwango cha 3G, 4G na kuendelea.



Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi, akijibu maswali ya yaliyoulizwa na baadhi ya wabunge Bungeni jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mchakato waanza ujenzi chuo Kikuu cha Teknolojia na Kilimo

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imeshaanza mchakato wa kukijenga Chuo Kikuu cha Teknolojia na Kilimo cha Mwalimu Nyerere Kampasi ya Butiama.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Omar Kipanga, alitoa kauli hiyo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Butiama (CCM), Jumanne Sagini.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji lini serikali itaanza rasmi ujenzi wa Chuo hicho.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema katika kutimiza azma hiyo, Serikali imetenga Dola za Kimarekani Milioni 44.5 sawa na Sh.Bilioni 103 kupitia mradi wa Mageuzi ya Kiuchumi kwa ajili ya Elimu ya Juu (Higher Education for Economic Transformation-HEET).

"Mradi wa HEET unatekelezwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na Benki ya Dunia kuanzia Septemba, 2021," alisema.

Alibainisha kuwa yapo baadhi ya maandalizi muhimu yaliyokamilika ambayo ni pamoja na kupatikana kwa Hati Miliki ya eneo lenye ukubwa wa Ekari 573.5, uandaaji wa Mpango kabambe, tathmini ya athari ya mazingira na usanifu wa majengo.

"Mheshimiwa Spika, kwa sasa taratibu zinazofuata ni kumtafuta Mshauri Elekezi na atakapopatikana atafanya kazi ya mapitio ya michoro, kuandaa hadidu za rejea na makabrasha ya zabuni ili kutangaza na kumpata Mkandarasi,"alisema.

Alisema michakato hiyo itakapokamilika ujenzi wa Chuo utaanza rasmi.

## Ataka kasi maboresho ya Sheria ya Mirathi

MBUNGE wa Viti Maalum (CCM), Husna Sekiboko ameitaka serikali kuharakisha marekebisho sheria ya masuala ya mirathi ili kuondoa tatizo la wasimamizi wa mirathi kuwadhulumu watoto na wajane.

Akiuliza swali bungeni jana, Mbunge huyo alisema wajane na watoto wamekuwa wakitaabika pale ambapo aliyechaguliwa kusimamia mirathi akijimilikisha mali hizo.

"Je, lini serikali italeta marekebisho ya sheria hii ili kuondoa changamoto hizi?, Je, Wizara inachukua hatua gani za dharura kuondoa changamoto hizi??"alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Geofrey Pinda, alikiri kuwa wakati wa vikao vya familia za marehemu wajane wamekuwa hawahusishwi kufikia mwafaka wa kupata msimamizi wa mirathi.

"Msimamizi wa mirathi sio mmiliki wa mali za marehemu, kwa kuwa sheria ya mirathi ina suala tatu inaruhusu mfumo wa kidini, kimila katika kugawa mali na sheria ya serikali kumekuwa na mkanganyiko mkubwa,"alisema.

Alisema kutokana na hali hiyo serikali imedhamiria kufanya mapitio ya taratibu hizo ili kuondoa mkanganyiko ambao ni janga kwa familia nyingi.

"Kila tunapokwenda maeneo mbalimbali ya nchi tunaelekeza na kutoa elimu kwa wahusika wote watambue wasimamizi wa mirathi sio warithi wa mali za marehemu, labda atajwe kwenye orodha ya mirathi lakini ataingia kwenye mgao wa kawaida wa mali,"alisema.

Alisema kuna tafsiri ambazo zinatokana na mfumo wa kikabila hali inayosababisha matumizi mbaya ya mali za marehemu.

Awali, Pinda alifafanua kuwa uteuzi wa Msimamizi wa mirathi hufanywa na kikao cha familia ya marehemu na aliyeteuliwa huthibitishwa na Mahakama.

"Kuendelea kwa vitendo vya dhuluma na udhalilishaji wa familia ya marehemu akiwamo mke na watoto, serikali imeanza kupitia upya Sheria ya Usimamizi wa Mirathi hiyo katika kubaini upungufu ili kurekebishwa,"alisema.

Alisema kwa kuwa chakato huo unahusisha taasisi za dini, mchakato umeanza wa kukutana nao na pia kukutana na viongozi wa makabila mbalimbali ili kupitia mila zao ambazo nyingi ni za udhalilishaji.

Hata hivyo, alisema ikibainika kutokea vitendo vya dhuluma kwa wanafamilia iliyompoteza baba wa familia inaelekezwa kwenda Mahakamani kutafuta haki zao.

"Nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge kutoa ushirikiano wa familia hizo ambazo nyingi hazina uelewa mkubwa wa masuala ya kisheria kufikia huduma hii ili waweze kupata haki zao,"alisema.





Ukurasa 13

Tumelikoroga, sasa tunayanywa


# BUFE

IJUMAA NOVEMBA 5 2021

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




**Kauli ya mabosi wahariri dhidi ya 'mdudu rushwa ngono'na vita vyake**

Ukurasa 12

WIKI YA FEDHA;- NOVEMBA 8 HADI 14…

# Wizara yajitokeza kueneza uelewa, ikiwa mbinu kukuza uchumi nchini

**Na Mwandishi Wetu**

INAPOFIKISHWA miaka 60 ya Uhuru wa nchi na kufanyika tafakuri kuhusu mafanikio ambayo yanapaswa kuyawekea mkakati mpya wa kipekee, ni eneo la sekta ya fedha.

Ni sekta yenye mchango mkubwa katika uchumi kuanzia wa mtu mmoja hadi taifa kwa ujumla. Kwa kipindi chote nchini kuna sheria na sera zinazosimamia Sekta ya Fedha, lakini udhaifu uliopo ni umma wa watu wengi nchini badi hawana uelewa mzuri kuhusu masuala ya fedha.

Sekta ya fedha ni muhimu katika umiliki wa uchumi, kwa maana haiwezekani mtu akaumiliki uchumi, bila ya kuwa na uelewa wa masuala ya fedha pamoja na uwezo au nafasi ya kupata fedha.

Kwa mfano, mtu akitaka kuanzisha mradi wowote uwe mkubwa au mdogo, anapaswa kuwa na fedha ambazo huenda atazipata kupitia mkopo kutoka taasisi za fedha au akiba aliyojiwekea kwa muda mrefu.

Udhaifu unaoonekana ni wa wananchi kukosa elimu ya taasisi za fedha na fedha kwa ujumla, hata wakatapeliwa na watu binafsi na mashirika mengine yasiyo rasmi kwa kuwalaghai kuwa watawakopesha, matokeo yake ni kukopeshwa kwa riba za juu na mwishowe ni kunyang'anywa mali walizoziweka kama nyumba, mashamba, viwanja, hivyo kuwarudisha nyuma kimaisha.

Wengine wanakimbilia kukopeshwa na matapeli kwenye mitandao na mwishowe ni kupewa masharti yakiwamo ya kutuma fedha, ili mikopo yao ishughulikiwe.

Hayo yote yamewaathiri wengi, hivyo kuilazimisha serikali kuanza kuchukua hatua; kubwa ikiwa ni kuanzishwa na kutekelezwa Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha kutoka mwaka 2021-2028/30.

Mpango huo umebeba mambo mengi, lakini, mpango mkakati wa utoaji elimu kwa umma ili Watanzania wengi wapate uelewa wa masuala ya fedha umepewa kipaumbele kikubwa na cha kipekee.

**MAKAMISHNA WA FEDHA**

Kamishna Msaidizi Fedha wa Wizara ya Fedha na Mipango, Dionisia Mjema, anasema umuhimu wa sekta hiyo ni kama damu katika meli binadamu na kwamba kama sekta hiyo haifanyi kazi, nchi yoyote haiwezi kuendelea, kutokana na umuhimu wake wa kuwa tegemea la kutoa mikopo kwa serikali na sekta binafsi.

Mjema anasema mpango huo, lengo lake ni kuifanya sekta ya fedha nchini kuwa imara na himilivu kutokana na mchango wake katika uchumi wa nchi na kwamba maeneo yanayoangaziwa ni benki, masoko ya mitaji, bima, hifadhi za jamii na huduma ndogo za fedha.

Anasema utekelezaji wa mpango huo kupitia mamlaka za usimamizi kama Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Mamlaka ya Usimamizi wa Bima (TIRA), Mamlaka ya Hisa na Mitaji (CMSA) na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mifuko ya Hifadhi za Jamii, utaifanya sekta ya fedha ikue na kutoa mchango katika uchumi na kuondoa umaskini.

Faida zingine zitakazotokana na utelekezaji mzuri wa mpango huo, ni uwezekano wa Tanzania kuzikopesha nchi nyingine zilizoko katika ushirikiano wa kikanda pamoja na udhibiti wa utakatishaji wa fedha.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Hata hivyo, Mjema anaeleza matumaini yake kuwa utekelezaji wa mpango huo utafikiwa na kuwanufaisha wananchi katika utumiaji wa huduma za fedha huku akitoa mfano jinsi Sheria ya Sekta Ndogo ya Fedha ya Mwaka 2016 ilivyoanza kuzaa matunda kutokana na uhamasishaji mkubwa uliofanywa.

Anasema, uhamasishaji huo umewezesha usajili wa vyama vya kuweka na kukopa (SACCOS) 460 tangu kuanza kutekelezwa, Vicoba 11,149 na na watoa huduma wengine za miamala ya fedha 549.

Janeth Hizza, Kaimu Kamishna Msaidizi Idara ya Kuendeleza Sekta ya Fedha, anaeleza kuwa utafiti wa mwaka 2017 ulibainisha kuwa asilimia 17 ya wananchi wanaotumia huduma za fedha, na kutokana na hali hiyo, serikali imeona wananchi wengi wapewe elimu ili wapate uelewa wa huduma za fedha zilizosimamiwa rasmi.

Hiza anaamini elimu itawapa uelewa wananchi kuhusu masuala ya fedha kwamba hata katika kukopa sio lazima kuweka dhamana ya nyumba au shamba bali mali nyinginezo kama madini na mifugo vinaweza kuwekwa kama dhamana ya kukopeshwa.

Makamishna Mjema na Hizza, wanasisitiza elimu kwa wananchi, ambayo imeanza kutolewa ikiyalenga makundi mbalimbali ya jamii.

Serikali inasema mkakati wa elimu utatolewa kwa miaka mitano ya kwanza, na kwamba kuanzia mwaka huu kila mwaka kutakuwapo na Maadhimisho ya Wiki ya Sekta ya Fedha, ambayo wananchi watakupatiwa elimu itakayotolewa na wataalamu wa wizara na taasisi zingine chini ya wizara hiyo.

Maadhimisho ya kwanza yanafanyika Viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam Novemba 8 hadi Novemba 14.

Kamishna wa Sekta ya Fedha, Dk. Charles Mwamaja, anasema, kutokana na umuhimu wa sekta ya fedha katika kuchangia maende-

**INAENDELEA UK 12**

# Kauli ya mabosi wahariri dhidi ya 'mdudu rushwa ngono' na vita vyake

- Ushuhuda wa ushindi kwa kujiamini
- Mwongozo, kazi na uwazi muhimu
- TAMWA yataja mzizi, suluhisho lake

**Na Jenifer Gilla**

GAZETI hili katika safu ya makala ilisharipoti hivi karibuni kuwapo madhila ya kijinsia katika vyombo vya habari. Ni hatua ya mchango wao kuripoti mambo yanayochangia ukombozi wa hali ya kijinsia.

Ni 'ajabu na kweli' vyombo vya habari navyo ni watumwa wa jinamizi hilo. Beatrice Bandawe, Mhariri Mtendaji wa gazeti la Nipashe anayekalia kiti hicho kwa saa 40 kila wiki, wastani wa saa nane kwa siku, anakiri kuwa mhusika wa kutafuta suluhisho la ugumu huo wa kiutawala.

Anasema mara zote ni mpokeaji mashitaka kutoka kwa wafanyakazi, anatatua migogoro, anakemea mienendo inayohatarisha usalama kazini, anashauri pamoja na kuelimisha.

Kwa miaka mitano aliyohudumu cheo hicho, Bandawe huwa anapokea malalamiko yasiyopungua matatu kwa wiki, lakini hakuna linalohusisha unyanyasaji kutoka kwa wanawake. Ni jambo linamloshangaza.

"Kesi za kijinsia ninazopokea hapa ni zile za mfumo dume, wanawake wakilalamikia kupewa kazi za aina fulani kutokana na jinsia zao," anaeleza, akiwa na ufafanuzi:

"Ya unyanyasaji wa kijinsia nimeshapokea na kutatua moja ya mwanaume kwa mwanaume, lakini ya mwanamke kwa mwanaume, bado sijapokea."



TAMWA ikiwa jijini mwanza kuwajengea uwezo wahariri, mameneja na wamiliki wa vyombo vya habari kuhusu usawa wa kijinsia na rushwa ya ngono ndani ya vyombo vya habari jana, mwaka huu :**PICHA :TAMWA**

Anarejea uchunguzi uliofanywa na shirika la Women in News kuhusu unyanyasaji wa kijinsia mwaka jana kwa nchi za kanda ya Jangwa la Sahara, ni kwamba kati ya wanawake watatu, mmoja ananyanyaswa kijinsia kwa vitendo

Pia, nusu yao wananyanyaswa kwa maneno, huku asilimia 15 ya wafanyakazi wanaume katika vyombo vya habari barani Afrika, wanatuhumiwa kuwanyanyasa wafanyakazi wanawake kingono.

Mkuu huyo wa gazeti Nipashe, anatoa uzoefu wake mkongwe katika vyombo vya habari, akikiri kuwapo kushamiri unyanyasaji kijinsia kwa wanawake, akiwa na ushuhuda wa simulizi za tabia zisizofaa kutoka kwa mabosi wa kiume.

"Unyanyasaji kijinsia upo, isipokuwa watendewa ni waoga kupaza sauti. Unakuta mkiwa nje ya ofisi, mfanyakazi wa kike anakutajia tabia za kinyanyasaji anazofanya bosi wa kiume, ukimuuliza kama alishamfanyia yeye, anakataa. Ukitaka kujua alimfanyia nani, pia hasemi anacheka tu,"anasema

Kwa mujibu wa Bandawe, kutopaza dhidi ya unyanyasaji huo, unaongeza chachu ya mabaya dhidi ya wahusika, hivyo hata jamii nje inakuwa haisaidii sana.

"Katika mazingira kama hayo, unashindwa kuchukua hatua kwa sababu inakuwa ni habari isiyo na uthibitisho. Sauti kutoka kwa watendewa ni muhimu sana," anasisitiza Bandawe.

Ni kauli inayoungwa mkono na Mhariri Mtendaji wa gazeti Nipashe Wikiendi, Epson Luhwago, anayesema katika miaka minne aliyohudumu cheo hicho, hajawahi kupokea ama kesi au malalamiko, ingawa anaona viashiria kutokana na maneno, pia matendo ya wahusika.

"Wakati mwingine unaona mfanyakazi wa kike anamchukia wa bosi wake wa kiume na anakuwa hayupo 'comfortable' (hana amani) akiwa karibu naye.

"Hapa unahisi kuna tatizo, ukijaribu kudadisi anakujibu 'changamoto za kawaida tumeshazizoea.' Sasa unashindwa kuingilia, kwa sababu unayehisi ananyanyaswa sio muwazi," anasema Luhwago.

**CHANZO NINI?**

Utafiti uliofanywa na Chama cha Wanahabari Wanawake (TAMWA), unaonyesha kuenea unyanyasaji wa kijinsia na rushwa ya ngono kwa wanawake, sababu kuu ni kipato kidogo kutoka kwa wanataaluma.

TAMWA inaeleza katika ripoti yake, kigezo hicho hutumiwa na mabosi kuwarubuni wanahabari kwa pesa za kukidhi mahitaji yao madogo.

Pia, wafanyakazi wapya watokao masomoni, hulagaiwa kutokana na hali yao ya chini kimapato na kutojiamini kikazi.

Kwanini hawaripoti udhalilishaji?

Bandawe anfafanua:"Waandishi wanawake wengi wananidhamu ya woga. Mtu anaona kuwa akimshtaki bosi wake, anaweza kuweka kibarua chake hatarini, wanaamua kuvumilia tu."

Katika hilo, Luhwago ambaye pia ni msaidizi wa Bandawe, anasema huwa wana hofu ya kufukuzwa kazi au jamii itawanyooshea kidole.

Mwandishi wa habari wa gazeti la Mwananchi Rachel Emmanuel (sio jina Lake Kamili), anakiri kukutana na unyanyasi kingono kazini (sio gazeti Mwananchi) lakini hakuripoti kwa kumhofia bosi huyo.

"Alikuwa na tabia na kukusifia viungo vyako vya siri na kuongea lugha inayodhalilisha na hufanya hivyo kwa wanawake tu. Mfano ukikosea, anakwambia 'muda wote unawaza kupaka vipodozi tu uvutie wanaume ndio maana hufanyi kazi vizuri.'

"Lakini, nilikuwa nashindwa kushitaki kwa sababu nilihofia kukosa nafasi gazetini, kama unavyojua sisi 'ma - correspondents' (waandishi wa kujitegemea) tunapambana walau kupata nafasi moja kwa siku kwenye gazeti" anasimulia kwa uchungu.

Mwenyekiti wa TAMWA, Joyce Shebe, anataja hofu hiyo ni zao la kutojengewa uwezo wa kuzungumza bayana ukatili waokutana nao kimamama wanahabari.

"Kwa sababu unyanyasaji kama wa kingono hufanyika kwa siri na hauna ushahidi na ukizingatia wanahabari wanawake hatujajengewa uwezo wa kuyazungumza wengi wao wanaogopa kusema pale wanapopitia hali hii", anasema.

Joyce, mzoefu wa chumba cha habari na Mhariri Mkuu huyo wa chombo Clouds Media Group, anataja kasoro pia ya viongozi kukosa elimu inayowasaidia kutoa taarifa aina hiyo.

"Sijawahi kuletewa mashtaka moja kwa moja isipokuwa unasikia tu mtu analalamika kuwa nimenyanyaswa, ila hanyooshi maneno kuwa anafanyiwa ukatili,"anaeleza.

Joyce anafafanua kuwa, hakuna namna bora ya kumsaidia kiongozi kupata taarifa za mwathirika, hivyo inakuwa ngumu hadi mhusika adadisiwe, ndio taarifa inapatikana, jambo lionalorejea haja ya viongozi kujengewa uwezo.

Anatoa ushuhuda wa utafiti wa kuwapa wanahabari wanawake karatasi waeleze changamoto zao, wengi waliadika adha ya udhalilishaji kijinsia.

Pia, anarejea kuwa baadhi ya wafanyakazi wa kike wanakosa nguvu ya kutoa taarifa wanaponyanyasika, kwa sababu huwa wanajitengenezea mazingira hayo.

Luhwago anaitafsiri hiyo, kuwa anachokiita 'uvivu na kutokujituma; kwa baadhi ya wanahabari wanawake, hata wakafuata mbadala wa kujirahishisha kwa mabosi.

"Unakuta mtu anataka awe anapangwa safari za mikoani au bungeni ili apate posho wakati utendaji wake wa kazi sio mzuri, anatumia jinsia yake kupata hizo 'favour'(upendeleo), madhara yake yanaangukia kwenye unyanyasaji na anashindwa kutoa taarifa," anasema.

Kwa wanaume, bosi huyo anataja shida kuu imekaa katika tabia mbaya.

**NINI KIFANYIKE**

Ramadhani Mbwaduke, mwanahabari mwandamizi anashauri waandishi wanawake wawe na bidii kazini, ili matunda ya kazi zao ziwaepushe kutoka hasi.

"Mahali popote pale wafanyakazi dhaifu ndio wanapitia kadhia hii. Kwa hiyo, nawasihi dada zangu kupiga kazi kwa weledi ili kusimama kwa kujiamini kukemea pale wanapoona dalili ya kutaka kunyanyasika.

"Kila mhariri anataka gazeti lake liwe na habari nzuri, hivyo hawezi kukataa story (habari) nzuri ya waandishi mwanamke, kwa sababu tu eti anamtaka kimapenzi," anasema mhariri huyo mzoefu kwa wastani muongo na nusu .

Beatrice anakazia hoja hiyo, akirejea alikotoka kwa ushuhuda wake binfasi kwamba hakunyanyasika kijinsia tangu anaanza taaluma hiyo, kwa sababu alijiamini, hakuchagua kazi na mara zote alivutia wahariri wake kwa kazi nzuri.

Baadhi ya wahariri wanaona, kuna haya ya kuwapo sera ya vyombo vya habari itakoyowapa nguvu wanahabari, Joyce Shebe akifafanua: "Inapaswa mtu anapoingia kazini au wale wanaokuja kwenye mafunzo kabla ya kuanza kazi aonyeshwe sera ya ndani inayoelekeza anapokutana na unyanyasaji wa kingono amuone nani au aripoti ofisi gani."BANGO LA TAMWA

Kwa miaka 34 TAMWA imekuwa mstari wa mbele kupambana na ukatili kijinsia, kwa kuielimisha jamii na kutoa taarifa za ukubwa wa tatizo kupitia njia kama vile vyombo vya habari, kongamano, warsha na semina na matunda yameanza kuonekana.

Mkurugenzi wa TAMWA, Rose Reuben, anajivunia juhudi hizo za elimu wanayotoa kwa muda mrefu, sasa inawaingia wanajamii katika vita dhidi ya ukatili kijinsia, kwani awali ilikuwa ya siri zaidi.

"Ile elimu tuliokuwa tunaitoa tangu chama kinaanzishwa imewaingia wanajamii na sasa ukatili wa kijinsia ukifanyika unazungumziwa hadharani tofauti na hapo awali ukatili wa kingono ili kuwa ni siri ya aliyetendwa, na hii inasaidia kuondoa suala janga hili", anasema.

Pia, anataja zao la Sheria ya Rushwa ya Ngono ya Mwaka 2017, inayowasaidia watu kupigania haki yao wanapoombwa rushwa ya ngono.

Mkurugenzi huyo anakumbusha mwaka 1998 wakati TAMWA pamoja na wadau wengine walipofanya kongamano la kukemea ukatili ulioshamiri kwa watoto, mabinti na kinamama, hata ikatungiwa sheria mahsusi dhidi ya Rushwa ya Ngono.

Hata hivyo, bosi huyo hakusita kutilia mkazo uelimishaji jamii kuhusu namna ya kuimaliza kabisa, akibebesha jukumu vyombo vya habari kubadilisha fikra za jamii, kwani inawasikiliza na kuwaamini.

## Wizara yajitokeza kueneza uelewa, ikiwa mbinu kukuza uchumi nchini

**INATOKA UK.11**

leo ya serikali imeandaa mpango wa miaka 10 kwenye mpango mkuu wa sekta ya fedha kutoka 2021-2029/30.

Mwamaja anasema, mpango huo umeweka kipaumbele katika kutoa elimu kwa umma kuhusu huduma za kifedha ili kukuza uchumi wa nchi pamoja na mtu mmoja mmoja.

Anasisitiza wanachotanguliza mbele ni faida zake, ambapo kuwa ni wananchi wengi kuzitumia huduma hizo kwa kukopa, kuwekeza pamoja na kukuza uchumi wa nchi.

**KATIBU MKUU**

Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, anasisitiza elimu ni kipaumbele katika kufanikisha mpango huo, huku akiviomba vyombo vya habari kuwaelimisha wananchi masuala ya kifedha, ili kukuza uchumi wa nchi.

Tutuba akizungumza na wahariri wa vyombo vya habari jijini Dodoma kwa ajili ya utoaji elimu, anaviomba vyombo vya habari nchini kulisaidia taifa kutoa elimu kwa wananchi kuhusu masuala ya huduma za kifedha kwa kuwa taarifa zao kufuatiliwa na jamii kila siku.

"Tumeona tuwajengee uwezo wa uelewa wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari hapa nchini ili kutoa elimu kwa wananchi wetu kuhusu masuala ya kifedha kwa sababu wanafuatilia taarifa zenu kila siku," alisema .

Anakiri kutambua umuhimu wa vyombo hivyo, katika kuelimisha umma wizara iliona ni vyema kutoa mafunzo kwa wahariri, ili elimu iwafikie wananchi.

Anasema Wizara ya Fedha, ina lengo la kutatua tatizo la uelewa wa wanachi kuhusu masuala ya kifedha, ili wajikwamue kiuchumi.

Kwa mujibu wa Tutuba, katika maadhimisho ya Wiki ya Sekta ya Fedha, wanatarajia kujielekeza katika kujenga weledi na uelewa umma kuhusu matumizi sahihi ya huduma za fedha na kuimarisha ufanisi wa masoko ya fedha .

Aliongeza kuwa wananchi watajengewa uelewa kuhusu kusimamia vizuri rasilimali fedha na kuwawezesha wajasiliamali wadogo kuongeza ujuzi sahihi wa matumizi ya huduma za fedha ili kukuza biashara zao.

Kadhalika alisema katika wiki hiyo wananchi watapewa elimu ya kuimarisha utamaduni wa kujiwekea akiba, kukopa na kulipa madeni kwa wakati.

Anahitimisha kwa ahadi ya kutumia machapisho, semina, maonyesho ya bidhaa za fedha na majukwaa ya kidijitali.

## TAFAKURI YA MLALAHOI

### Tumelikoroga, sasa tunayanywa





**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: jkulangwa@yahoo.com

NILIPATA kusema kwenye safu hii kwamba, Wamachinga wanachokitaka si matiti, bali maziwa. Kwamba hawajali watayanywea kwenye kikombe, chupa au kopo, ili mradi ni maziwa safi na salama.

Nilimaanisha kuwa vijana wetu hawa wanachotaka ni maeneo wanakoweza kuyapata hayo maziwa, wakanywa na kusaza, lakini na maisha yao kiafya yakawaruhusu kusonga mbele.

Kwamba wanahitaji maeneo mazuri ya kufanyia biashara zao. Maeneo hayo si majumba yenye vioo, maeneo hayo si majumba yenye viyoyozi, wala si yenye viti vya sofa.

Wanahitaji maeneo yenye wanunuzi wa bidhaa zao. Wanunuzi hao ndiyo maziwa yenyewe. Ukiwapeleka mahali pasipo na wanunuzi ni sawa na kuwapa matiti yasiyo na maziwa.

Na tunajua mtoto ukimpa titi lisilotoa maziwa, bila shaka ataling'ata tu. Wamachinga katika baadhi ya mikoa wameanza kung'ata matiti wanayopewa, kwa sababu hayatoi maziwa.

Wanang'ata, kwa sababu tulishawaaminisha kuwa mama aliyewapakata ana matiti yanayotoa maziwa. Ni kweli waliamini baada ya kuminya matiti na maziwa yakatoka.

Matiti hayo ni yale yaliyo mitaa kama Kongo na mingineyo katikati ya Jiji la Dar es Salaam na mitaa kama hiyo katikati ya majiji ya Mwanza, Arusha, Mbeya na mingine. Kwanini wasing'ang'anie matiti?

Kama mjuavyo, mtoto akinyonya matiti yanayotoa maziwa mengi na akashiba, matokeo yake ataanza kuyaminyaminya na maziwa kuchuruzika, naye kuona ni mchezo.

Sasa ndivyo walivyofanya Wamachinga wetu hawa wakanyonya na kuminya maziwa, huku pia kinamama wenye matiti yao nao wakichekelea na kuwapiga piga mgongo kama kuwapongeza vile. Ndiyo sababu tukashinikiza kuwa waacheni Wamachinga, msiwabughudhi. Waacheni wanyonye mpaka wachezee matiti ya mama zao, waacheni wachezee maziwa yanayochuruzika. Ndiyo sababu ya vitambulisho vya shilingi 20,000.

Wakati wakiendelea kunyonya na kusaza na kuminyama titi huku maziwa yakichuruzika, mnakuja mnaua mama zao. Mama akifa hata kama ana maziwa mengi kwenye matiti hayatachuruzika kamwe.

Mnawapeleka mahali penye matiti, lakini yasiyo na maziwa. Walishazoea kunyonya mbele ya maduka ya matajiri, walishazoea kunyonya juu ya mitaro na makaravati.

Tulishawahakikishia mama zao wenye matiti yaliyoshehеni maziwa, nao wakituhakikishia kura kila baada ya miaka mitano, kila uchaguzi. Tukiwaita wanyonge wapiga kura wetu hawa.

Nao wakajiona kweli ni wanyonge wapiga kura wenye uhakika wa kuendelea kushikilia na kubinya matiti yenye maziwa miaka nenda rudi. Sasa ghafla mama zao (vibanda) wanashambuliwa na kuuawa wakishuhudia.

Kilio chao kisikilizwe ili watafutiwe kinamama hata wa kukodi, ili mradi wana maziwa kwenye matiti yao basi wanyonye.

Nimesema hawajali maziwa yanatoka kwenye sufuria, chungu, chupa, kopo au bakuli hata beseni.

Ili mradi wao wanyonye maziwa wayatakayo. Kujenga masoko ya maghorofa, kujenga stendi ya maghorofa, kisha uwaambie nendeni huko, kama hakuna biashara huko, ni kwamba wanaangukia kitendawili cha kunywa chai ya maziwa na si maziwa yenyewe.

Binafsi nadhani kwa kurejea tulikotoka, kamwe hatukustahili kuwa taifa la Wamachinga wakati ardhi kubwa tunayo.

Naguswa na kusuasua uchukuaji wanafunzi kuhudhuria mafunzo ya Jeshi la KujengaTaifa (JKT), nikiona uhusiano wake na wimbi la vijana kukimbilia mijini kusaka ajira. Kumbukeni wimbo wa Gezaulole ulioimbwa na bendi ya Urafiki Jazz. Mtakumbuka Kibugumo na Mwanadilatu kwenye makao mapya?

Kwamba jembe ndiyo satifiketi ya mwana wa mapinduzi na mtu mwenye busara. Kilimo, kilimo, kilimo! Tukaacha kupeleka vijana JKT wakati fulani, sijui ni kwa sababu zipi?

Kwa yeyote aliyepitia mafunzo ya JKT, atakubaliana nami kwamba kama tungeendelea na wazo lile la JKT wa kujitolea wakaenda wakaanzisha mashamba kama ilivyokuwa enzi hizo na kuzalisha mazao. Haya ya Wamachinga tungeyasikia tu.

Leo tunafukuzana mitaani, kwa sababu tu hatukuwa na mipango mikakati sahihi ya kuwatumia vijana wetu wanaomaliza elimu zao na kuendelea kuwashawishi kujiajiri.

Hivi sasa wanajiajiri kwa kuuza plastiki na nguo za mitumba mitaani! Wamachinga watambuliwe haki zao kusaudia Kazi Iendelee! Alamsiki!

FEDHA

# Wanachama UTT AMIS wafunguka namna mfuko wao unavyowabadilishia maisha

## • Rasmi Zanzibar ikiwa ni ya kipekee
## • Wastaafu waja na simulizi zakwao




Mkurugenzi Mtendaji wa UTT AMIS, Simon Migangala (kulia) na Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa asasi hiyo, Juma Muhimbi. **PICHA ZOTE: MPIGAPICA WETU.**

**Na Frank Monyo**

UNAIJUA asasi UTT AMIS? Ni taasisi inayosimamiwa na serikali ikiwa na umri zaidi ya miaka 10 chini ya usimamizi Wizara ya Fedha na Mipango, jukumu lake kubwa ni kuwahudumia Watanzania wenye vipato vya chini kuwekeza kwa manufaa yao, familia na taifa.

Ofisa Mwandamizi wa Masoko na Uhusiano wa kampuni hiyo, Rahim Mwanga, anasema serikali iliweka wigo mpana kwa umma, ikiweka akiba na kuwekeza kwenye masoko ya fedha na mitaji, ili kushiriki vyema katika kumiliki uchumi nchini, ndani ya mabadiliko ya sera zake.

Rahim anasema, ndani ya mwaka mmoja uliopita sasa, wanazidi kuwafikia wengi, wakifungua ofisi Unguja miezi mwili iliyopita na kuna matawi katika mikoa ya Mbeya, Dodoma, Mwanza na Arusha.

Mwanga anaeleza UTT AMIS inaboresha mifumo yake sasa kupitia simu za kiganjani, ili kumwezesha mtu kujiunga na kupata taarifa za uwekezaji, kwa kupiga katika anuani maalum ya simu (*150*82#) au upakuaji (UTT AMIS).

Hadi sasa ina jumla ya mifuko sita ambayo ofisa huyo anazitaja ni: Umoja, Watoto, Wekeza Maisha, Kujikimu, Ukwasi na Hati Fungani, akisema ni mageuzi yanayokabili ugumu wa umma katika namna wavyotaabika kufikia masoko ya fedha na mitaji.

**INAFANYAJE KAZI?**

Mwanga anasema UTT AMIS imepewa leseni na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), kukusanya amana kutoka kwa wawekezaji na kuziwekeza.

"Tukishapata hizo fedha tunaenda kuwekeza katika mfuko husika, kulingana na waraka wa toleo la mfuko. Mifuko yetu tuliyo nayo inawekezwa katika sehemu kubwa mbili; masoko ya fedha na masoko ya mitaji.

"Faida inayopatikana inarejeshwa na kugawanywa kwa wawekezaji na sehemu ya uwekezaji wao katika mfuko, ndio inafahamika kama kipande," anafafanua Mwanga.

Anataja masoko husika yanahusisha dhamana za uwekezaji zaidi ya mwaka mmoja, akitoa mfano katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE), pia hati fungani ama za muda mrefu serikali au ambazo mwekezaji anaikopesha muda mrefu na baadaye inamlipa kwa mujibu wa makubaliano.

**FAIDA IKOJE?**

Mwanga anaendelea mifuko ya uwekezaji inawapa fursa wenye mitaji midogo kuwekeza kwenye masoko ya fedha na mitaji, kwa viwango vidogo, pia kila mara.

Pia, kampuni ya UTT AMIS imekuwa ikitoa elimu ya fedha kila mara kwa makundi tofauti na namna ya kuwekeza katika mifuko yao, kwa malengo ya baadaye, sambamba na elimu ya kukabiliana na athari za baadaye kwenye biashara na maisha.

Mmoja wa wanufaika wa elimu ya uwekezaji inayotolewa na UTT AMIS, Fadhili Mohamed,(79), mkazi wa Mwanakwerekwe Zanzibar, anasimulia manufaa ya darasa la uwekezaji, kwamba amenufaika na elimu uwekezaji kutoka UTT AMIS, hata maisha yalivyobadilika baada ya kupata kiinua mgongo alipostaafu.

Anakiri amenusurishwa na mwelekeo wa kuwa ombaomba, akirejea mifano ya wastaafu wengi waliofuja pesa zao na kushindwa kutimiza malengo.

Fadhili anasema baada ya kupata elimu, aliamua kuwekeza kwenye 'Mfuko Wekeza Maisha' kwa malengo ya miaka 10, ikiambatanishwa na faida za bima.

Anasema mwekezaji katika mfuko huo, anaweka lengo la kiasi anachotaka kuwekeza kwa miaka 10, cha chini Sh. milioni moja, akiwa na hiari ya kuwekeza kwa mkupuo au awamu.

"Mtu ukichagua kuwekeza kiasi hicho (Sh. milioni moja) kila mwezi atahitajika kuwekeza kiasi cha Sh. 8,340 tu ili kukamilisha mpango wake wa uwekezaji.

"Zaidi ya asilimia 99 ya fedha za mwekezaji huwekezwa na chini ya asilimia moja hutumika kugharimia bima," anasimulia, akitaja aina ya bima hizo ni za maisha, ulemavu wa kudumu na ajali.

Mohamed anasimulia baada ya miaka 10, alifungua kiwanda cha kuzalisha mkaa mbadala, huku akifanya shughuli za kilimo cha mwani na karafuu, akijivunia mafanikio makubwa kupitia elimu aliyoipata UTT AMIS kuhusu matumizi ya fedha.

Ofisa wa UTT AMIS - Mwanga, anafafanua lengo la Mfuko wa Jikimu ni kukuza utoaji gawio na mapato ya ziada kwa vipindi tofauti, pia kumkuzia mwekezaji mtaji.

Anasema mfuko unatoa fursa mbili za uwekezaji, mapato ya robo mwaka, pia mwaka mzima, kwa kuambatanisha na ukuaji vipande.




Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mhandisi Hamad Yussuf Masauni, akizungumza na wanachama wa UTT AMIS Zanzibar, alipozinduza ofisi yake, Agosti mwaka huu .

Kiwango cha chini cha uwekezaji katika mfuko huo kwa Mpango wa Mapato ya Robo Mwaka, ni Sh. milioni mbili; milioni moja kwa Mpango wa Gawio kwa Mwaka; pia Sh. 5,000 kwa Mpango wa Ukuaji Mtaji kwa Mwaka.

"Kiwango cha chini cha uwekezaji wa nyongeza au unaofuata (additional investment) ni Sh.15, 000 kwa mpango wowote wa gawio na Sh.5, 000 kwa mpango wa ukuaji mtaji kwa mwaka, hakuna ukomo wa kiwango cha kuwekeza," anafafanua.

**WANUFAIKA KIBIASHARA**

Mwekezaji Faudhia Jumaa, mkazi wa Mpendae, Zanzibar anaelezaa: "Nilikuwa na ndoto ya kufanya biashara ya kuagiza bidhaa kutoka nje ya nchi, lakini baada ya kuibuka kwa janga la corona, mipaka ikafungwa na biashara zikasimama.

"Kwa hiyo, ile pesa niliyotaka kuagizia mzigo ikanibidi niwekeze katika Mfuko wa Ukwasi, huku nikisubiri hali ikae sawa."

Anaeleza elimu ya kuweka akiba na kuwekeza aliyopewa na kampuni ndiyo iliyompa mwanga katika safari yake kuwa mfanyabiashara mkubwa, pesa alizowekeza UTT AMIS zimemuongezea mtaji.

Faudhia anataja manufa ya fedha hizo, imemuwezesha kufungulia watoto wake akaunti katika Mfuko wa Watoto kupitia Benki ya CRDB.

"Nilijiunga na Mfuko wa Watoto na kuanza kununua vipande kupitia Benki ya CRDB kwa ajili ya ada ya watoto wangu na mahitaji ya shule, kila mmoja nilimfungulia akaunti yake," anasema Faudhia, akitaja sehemu ya manufaa ya uwekezaji huo una kiwango cha chini, Sh. 10,000.

**MNUFAIKA MSTAAFU**

Juma Songoro, mstaafu kutoka taasisi ya kiserikali, anayesema UTT AMIS imemsaidia kutunza fedha zake za kiinua mgongo kwa faida, akitafiti biashara ya kufanya.

Anasema kiinua mgongo chake amekiwekeza katika mfuko wa Hatifungani. Anafafanua: "Niwatafuta UTT AMIS kwa ajili ya kupewa elimu ya uwekezaji na jinsi mifuko yao inavyofanya kazi na nikaamua kuwekeza Sh. milioni 50 ambayo kwa mwezi nikawa napokea wastani wa Sh. 500,000, inayonitosha kabisa."

Mwenyekiti wa Kikundi cha Uwakiba kilichopo Dar es salaam, Saidi Mwarami, anasema wawekeza kwenye UTT AMIS kwa zaidi ya miaka minne sasa.

Anataja manufaa ni kuendesha miradi mbalimbali, ikiwamo ufugaji wa samaki, wakichanga kila wiki na kuna mchango mkubwa wa mwezi, fedha hizo wamekubaliana wanachama wote kutoa asilimia 10 kwa kila michango itakayopatikana na kuwekeza kampuni ya UTT AMIS kupitia mfuko wa Ukwasi.





# RC ataka kuanzishwa klabu wapinga rushwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Antony Mtaka, amezindua mafunzo ya mwongozo wa wawezeshaji kufundisha vijana wa skauti elimu ya rushwa huku akisisitiza klabu za wapinga rushwa kuanzishwa katika shule na vyuo vyote mkoani Dodoma.

Akizungumza wakati akizindua mwongozo huo, Mtaka alisema lazima Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ipanue wigo zaidi kueneza elimu ya rushwa kwa makundi mengine.

"Nipongeze ushirikiano huu utasaidia sana kuenea kwa elimu hiyo. Skauti ni vijana wazalendo, hivyo elimu ya rushwa wanayoipata itaenea zaidi na ni watu sahihi katika kutoa elimu hii.

"Hapa Dodoma tuna shule takribani 1,000. Hizi shule zote zikiwa na klabu za wapinga rushwa tutakuwa na kizazi kizuri cha baadaye kinachochukia rushwa na si kufundishwa elimu ya rushwa mtu akiwa tayari kaajiriwa," alisema Aliitaka TAKUKURU kuongeza elimu hasa kwa wanafunzi katika ngazi za chini kwa kuwa ndio waajiri na waajiriwa wa baadaye na kwamba elimu ikitolewa itapunguza kwa kiasi kikubwa vitendo vya rushwa na kujenga kizazi chenye maadili.

"Unajua kwa nini Ukristo na Uislamu havifi? Ni kwa sababu wamewekeza tangu watoto wanakuwa na kufundishwa. Vivyo hivyo kwenye rushwa mkiwekeza kikamilifu kwa wanafunzi mtajenga jamii imara inayochukia rushwa," alisema.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema wameamua kuwapa mafunzo vijana wa skauti kwa kuwa misingi na wajibu wao ni uzalendo, uwajibikaji na uadilifu, hivyo wakipewa mafunzo litakuwa jambo jema kwa kueneza elimu hiyo kwa jamii.

"Ukiangalia misingi ya Skauti kwanza ni kundi la watoto miaka mitano hadi hadi 26. Tuliona hili ni kundi muhimu na ukizingatia misingi ya kazi zao tukaona ni watu sahihi wa kutoa elimu ya rushwa katika Mkoa wa Dodoma," alisema Kibwengo

Alisema katika mafunzo hayo, watatoa mada mbalimbali kwa vijana wa skauti ikiwamo TAKUKURU na ushirikishwaji wa umma katika mapambano ya rushwa, misingi na mbinu za skauti kujenga uzalendo, uadilifu na uwajibikaji, muundo wa matumizi ya mwongozo wawezeshaji kujenga uzalendo uadilifu na uwajibikaji kwa vijana wa skauti. Alisema katika kuendelea kutoa elimu ya rushwa wamefanya semina mbalimbali katika makundi mbalimbali na kufungua klabu 26 mpya katika shule na vyuo na kuendelea kuimarisha klabu za wapinga rushwa ili kupanua wigo zaidi wa utoaji wa elimu ya rushwa.

"Elimu tunayotoa imesaidia sana kama unavyojua tulitoa elimu katika ofisi za umma na binafsi kuwa na mifumo ya kushughulikia vitendo vya rushwa imeanza kuzaa matunda ambapo tumeona chuo kikuu cha Dodoma mkufunzi aliyekutwa na kosa la rushwa ya ngono kachukuliwa hatua" alisema.

# 70% vyuo vikuu watoka sekondari kata

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), anayeshughulikia Elimu, Gerald Mweli, amesema shule za kata zilizokuwa zinabezwa kwa sasa zinachangia zaidi ya asilimia 70 ya wanafunzi kwenye vyuo vikuu nchini.

Aidha, amesema serikali imejipanga kutatua kero mbalimbali kwenye sekta ya elimu ikiwamo walimu wa masomo ya Sayansi na Hisabati ili wanafunzi wamudu masomo hayo.

Mweli aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akifunga Mkutano wa Mwaka wa Wadau wa Elimu waliokutana kutathmini hali ya elimu na kuweka mikakati mipya ya namna ya kuboresha sekta hiyo.

Alisema wakati shule hizo zinajengwa zilibezwa sana lakini zimekuwa na matokeo chanya kwa jamii na kwamba imani ya serikali ilivyoanzisha shule za kata ndiyo hiyo iliyopo kwenye elimu ya msingi bila malipo.

"Sisi tulipoamua kama serikali mwaka 2005/6 kujenga shule za kata tulisemwa sana lakini kwa sasa zinapeleka zaidi ya asilimia 70 ya wanafunzi vyuo vikuu. Shule tatu za kata kwenye matokeo yaliyopita ziliingia 10 bora kidato cha sita na hizi zinazoingia hazichukui wanafunzi bora wao wanapangiwa wanafunzi wanaenda na wanaibuka na daraja la kwanza wote," alisema.

Kuhusu uhaba wa walimu, alisema: "Kwenye mitihani mingi hata huu wa juzi wa darasa la saba somo la Kiingereza hawajafanya vizuri sana. Mmejadili hapa na kuzungumza kwa mapana yake. Ukiangalia mwezi Juni, Rais Samia Suluhu Hassan alivyotoa ajira za walimu 3,000 walikuwa walimu wa hisabati na sayansi. Si kwamba walimu wa sanaa hawana umuhimu bali tulikuwa tunahitaji zaidi walimu wa sayansi."

"Mtakumbuka miaka mitatu minne iliyopita tulikuwa tukikutana namna hii tukaambiwa tunaajiri walimu lakini tunawapanga kwenye shule zisizo na mahitaji. Mwaka huu walimu walikuwa wanaajiriwa kwa kuchagua shule wenyewe na kwenye mfumo zilikuwapo shule zenye uhitaji tu," alisema.

Mweli pia alisema serikali imejipanga kuondoa adha kwa wanafunzi shule za msingi kutembea umbali mrefu kwa kujenga madarasa 3,000 katika vituo shikizi 970 na kuzisajili kuwa shule kamili.

"Tunaamini tukishajenga madarasa 3,000 kwenye hivi vituo shikizi 970, tunakwenda kuweka historia tena kubwa kwa shule hizi za msingi mpya 970. Pia tutakuwa tumewaondolea adha kubwa watoto kutembea umbali mrefu watoto wanatembea kilometa 20 hadi 60 kufuata shule kwenye maeneo mengine,"alisema. Naibu Katibu huyo alisema katika suala la udhibiti ubora wa elimu, serikali imefanya makubwa kwa sasa idara hiyo na kuwataka wadau na wazazi kuitumia idara hiyo ipasavyo ikiwamo kujua kazi zinazofanyika katika shule hizo.

Aliwahakikishia wadau kuwa serikali ilishaanza kuyafanyia kazi maoni waliyotoa na kuwataka wadau kuendelea kutoa ili kuboresha sekta ya elimu.

Naye Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Prof. James Mdoe, alisema katika mkutano huo wamefanya tathmini ya utendaji katika sekta hiyo kwa kujumuisha serikali, wadau wa mashirika yasiyo ya kiserikali na wahisani.

Mkurugenzi wa Shirika lisilokuwa la kiserikali la Karibu Tanzania Organization, Majid Mjengwa, alisema kuna mafanikio makubwa kwenye sekta hiyo hasa shule za kata ambazo zimeleta mapinduzi makubwa kwa kuzalisha wanafunzi wengi kwenda vyuo vikuu licha ya awali zilibezwa.



Mchungaji Kiongozi wa kanisa la Talatha Cimu mkoani Dodoma, Daniel Kitua, akichangia damu katika maadhimisho ya sikukuu ya Chama cha Wanaume wa kanisa hilo, jijini Dodoma juzi. Anayemhudumia ni Muuguzi Asha Mohamed kutoka Mpango wa Taifa Damu Salama Kanda ya Kati. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Serikali yaombwa kasi anwani za makazi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKATI dunia ikiwa inakabiliwa na janga la corona, wadau wa masuala ya Teknolojia ya Habari na Mawasilino (TEHAMA) nchini, wameiomba serikali kuharakisha mchakato wa usambazaji wa anwani za makazi ili kurahisisha utoaji wa huduma.

Rai hiyo ilitolewa jana jijini hapa na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya MhawaNet ICT Solutions, Simon Chagula, wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya uzinduzi wa ofisi ya utoaji huduma mbalimbali za masuala ya TEHAMA.

Alisema kutokana na dunia hivi sasa kukabiliwa na janga la corona, kumekuwapo na fursa nyingi hasa katika masuala ya teknolojia ya habari na mawasiliano.

"Kwa mfano tangu janga la corona liingie, mawasiliano mengi yamekuwa yakifanyika kwa njia ya mtandao. Watu wengi kupitia TEHAMA wamekuwa wakifuatilia madhara yanayotokea kwa nchi zingine hususani mataifa ya Ulaya na Amerika ambako madhara makubwa yameonekana," alisema.

Pia alisema hivi sasa watu wengi hawasafiri kutoka eneo moja kwenda lingine kutokana na janga hilo, hivyo TEHAMA imekuwa ikitumika katika kusafirisha huduma mbalimbali zikiwamo bidhaa.

"Hivi sasa watu hawasafiri hivyo hata wafanyabiashara wanatumia TEHAMA kufanya kazi zao kwa kutumia mitandao kuwafikia wateja wao," alisema

Chagula alisema kutokana na hali hiyo serikali inatakiwa kuwekeza katika usambazaji wa 'PostCode' na anuani za makazi ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa njia ya TEHAMA.

"Hivi sasa watu wanatumia mitandao kuagiza bidhaa mbalimbali lakini ili imfikie mtu lazima kuwapo na anuani za makazi za uhakika, hivyo serikali inatakiwa kurahisisha mchakato huu ili watu waendele kupata huduma kama kawaida licha ya uwepo wa janga la corona," alisisitiza na kuongeza kuwa katika miaka ya hivi karibuni, dunia bila teknolojia haiwezi kwenda.

"Hivyo basi uzinduzi wa ofisi hii inayojishughulisha na masuala ya TEHAMA, utasaidia zaidi taasisi za serikali, taasisi binafsi na watu wengine hususani vijana kuijua Dunia kwa muda mfupi" alisema

Pia alisema ofisi hiyo itawasaidia wakazi wa jiji la Dodoma, mikoa mingine na nchi jirani kupata huduma za TEHAMA ikiwamo uundwaji wa program na uhifadhi na kulinda mifumo ya TEHAMA.

Kadhalika masuala ya 'graphic design' na matangazo, utengezaji wa vifaa mtambuka vya TEHAMA, kununua vifaa vya TEHAMA na kupata ushauri wa matumizi bora na salama ya vifaa na mifumo ya teknolojia hiyo.

Alisema ofisi ya MhawaNet ICT Solutions inaunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa ajira kwa vijana wa Kitanzania ambapo tayari wametangaza nafasi za ajira katika kada mbalimbali.



# Aliyehukumiwa miaka 30 jela kwa ubakaji mwanafunzi aachiwa huru

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mbeya, imemwachia huru Peter Mlelwa (46) mkazi wa Nsalaga, Uyole jijini Mbeya, baada ya upande wa mashtaka kushindwa kuthibitisha mtu huyo kumbaka na kumpa ujauzito mwanafunzi wa shule ya msingi.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi na Hakimu Mkazi Andrew Scout baada ya kusikiliza ushahidi wa mashahidi wawili wa upande wa Jamhuri na pia upande wa utetezi kwenye kesi hiyo ambayo ni rufaa baada ya hapo awali mtu huyo kuhukumiwa kifungo cha miaka 30 jela kwa kuonekana kuwa alimbaka na kumsababishia ujauzito mwanafunzi huyo.

Hakimu Scout alisema amemwachia mshtakiwa kutokana na upungufu wa kisheria, hivyo kukosa uthibitisho wa wazi kwamba ni kweli mshtakiwa alimbaka mwanafunzi huyo na ikiwa ndiye alimpatia ujauzito mtoto huyo.

Alisema miongoni mwa sababu za kumwachia huru Mlelwa ni mwathirika kutomtaja mshtakiwa kama ndiye mtu aliyembaka badala yake baada ya kugundulika kuwa mjamzito baada ya miezi saba ya ujauzito alidai mahakamani kwamba alibakwa na Baba Dori bila kumtaja jina.

Pia alisema upande wa mashtaka haukumpeleka mahakamani daktari kuwa shahidi wao ili kuthibitisha madai hayo wala kielelezo muhimu ambacho ni fomu namba tatu ya polisi kwa ajili ya matibabu.

Awali, ilielezwa kwamba mtoto huyo hakuwa na akili nzuri bila kubainisha ukweli kisheria kupitia maandishi au utaalamu maalumu kudhihirisha matatizo hasa ya afya ya akili lakini kwenye usikilizwaji upya wa kesi hiyo, imethibitika ana akili nzuri isipokuwa ana matatizo kwenye miguu na mikono.

Kutokana na upungufu huo wa kisheria, Hakimu Scout amemwachia huru mshtakiwa huyo ambaye alikuwa mrufani.

Mshtakiwa alikuwa akishtakiwa na Jamhuri kwa tuhuma za kumbaka mwanafunzi wa shule ya msingi mwenye umri wa miaka 16 (jina linahifadhiwa)) Aprili, 2019 huko Nsalaga kosa ambalo ni kinyume na kifungu namba 130 (1), (2) E na 131 na shtaka la pili kumpa ujauzito mwanafunzi huyo kinyume na kifungu namba 60 A (3) cha Sheria ya Elimu namba 353.

Baada ya kusikilizwa kwa shauri hili namba 252/2019 awali, mshtakiwa huyo alikutwa na hatia, hivyo kuhukumiwa kifungo cha miaka 30 jela.

Kupitia rufani yake, ameachiwa huru baada ya kesi dhidi yake kutothibitishwa bila kuacha shaka yoyote kama sheria inavyoelekeza.




Ofisa Uhifadhi Utalii wa Hifadhi ya Ruaha, mkoani Iringa, Amina Salum akifafanua jambo kwa waandishi wa habari, wakati wa ziara waliyoifanya juzi, kwa lengo la kuvitangaza vivutio mbalimbali vya utalii vinavyopatikana hifadhini hapo. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Waomba kupatiwa vibali uchimbaji madini

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

TAASISI ya Maendeleo ya Viziwi Tanzania (CHAMAVITA), imeomba serikali kuwapatia vibali vya uchimbaji madini katika migodi watu wenye ulemavu ili kurahisisha shughuli zao.

Ombi hilo lilitolewa juzi na Mtendaji Mkuu wa (CHAMAVITA), Kelvin Nyema, wakati wa warsha ya kuwajengea uwezo viziwi wanaojihusisha na shughuli za uchimbaji madini kutoka Mikoa ya Mbeya na Songwe ambayo yaliandaliwa na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO).

Nyema alisema kutokana na vikwazo wanavyokabiliana navyo, wameiomba serikali kuwatengea eneo lao ili kufanya shughuli zao kwa utulivu.

"Tunakabiliwa na vikwazo mbalimbali wakati tunatimiza majukumu yetu ya uchimbaji madini ya dhahabu serikali imetusahau tunaomba kuwezeshwa kiuchumi, vitendea kazi na maeneo rasmi ya uchimbaji," alisema Nyemo.

Wakizungumza na Nipashe, wachimbaji hao walisema licha ya kupatiwa elimu ya teknolojia za kisasa za shughuli za uchimbaji wa madini na uchenjuaji pia wanahitaji kupatiwa maeneo maalum kwa ajili ya kufanyia shughuli zao ili kuepukana na usumbufu wanaoupata kutokana na miundombinu ya migodini kutokuwa rafiki kwao.

Miongoni mwa wachimbaji hao, Mariam Afyusisye kutoka mkoani Songwe alisema serikali kupitia Waziri ya Madini ilitizame kundi hilo kwa jicho la huruma kwa kuwapatia maeneo ya uwekezaji kwani wengi wao ni vibarua na wamekuwa wakinyanyasika kutokana na ulemavu walio nao.

Yassin Tembo, kwa upande wake aliomba serikali kulifanyia kazi ombi lao kwa kuwa wamekuwa wakitegemea shughuli za uchimbaji wa madini na kufanya vibarua kwenye migodi ili kupata fedha za kujikimu na familia zao licha ya kuwa na tatizo la uziwi.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, alilihamasisha kundi hilo kujiunga kwenye vikundi ili kupatiwa mikopo kutoka katika halmashauri ikiwamo kupatiwa vifaa vya kisasa vitakavyorahisisha shughuli za uchimbaji wa madini.

Meneja wa wachimbaji wadogo ambaye pia ni mlezi wa wachimbaji kutoka STAMICO, Tuna Bandoma, alisema watalishughulikia ombi hilo.

Alifafanua kuwa utaratibu wa wachimbaji maeneo mengi nchini huwa wanatafuta kulingana na jiolojia mbali ya yaliyoyengwa na Serikali na kwamba kutokana na umuhimu wa kundi hilo watafanya kila namna ya kupata mwarobaini.

# Rufani aliyefungwa kwa kubaka mkewe yagonga mwamba

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mbeya, imetupilia mbali kesi ya rufani ya Shauri Vungwa (40) mkazi wa kijiji cha Mamba wilayani Chunya, aliyehukumiwa na Mahakama ya Wilaya ya Chunya kifungo cha maisha jela baada ya kukutwa na hatia ya kumbaka aliyekuwa mke wake na kumnyofoa kizazi.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi na Hakimu Mkazi Mfawidhi, Zawadi Laizer, baada ya kusikiliza maombi ya mleta rufani huyo.

Hakimu Laizer, mwenye mamlaka ya nyongeza kusikiliza kesi hiyo ya rufani, alisema amepitia kwa umakini hoja saba za mleta maombi kupinga adhabu ya kifungo cha maisha jela ikiwamo madai kwamba alionewa kwa kuwa mahakama ya wilaya haikuwa na weledi kutoa uamuzi huo na kwamba Jamhuri imeshindwa kuthibitisha ipasavyo kuwa alimbaka mwanamke huyo aliyekuwa mkewe.

Alidai sababu nyingine ni mleta maombi haikuwa na uhakika kwamba yeye ndiye alimwingilia mwanamke huyo kwa kuwa tukio lilifanyika usiku majira ya saa tano kasoro. Pia alidai kuwa kesi hiyo ilitengenezwa dhidi yake, hivyo pamoja na sababu zingine, aliiomba mahakama kumwachia huru.

Akitoa uamuzi, Laizer alikiri kwamba mahakama ya wilaya ya Chunya ilitoa adhabu ya juu ya kifungo badala ya miaka 30 ambayo sheria inaelekeza kwa kosa la ubakaji bila hakimu kueleza sababu za kutoa adhabu hiyo.

Aliongeza kuwa kutokana na mazingira ya tukio kwamba mleta maombi alimwingilia kimwili mwanamke huyo mwaka 2017, ikiwa miaka miwili tangu walipotengana, ilielezwa kuwa aliingiza mkono wake sehemu za siri za mwanamke huyo na kumvuta kizazi hali iliyomsababishia maumivu makali.

Laizer alisema kwa mamlaka ya mahakama yake na kulingana na matukio hayo ya kikatili kuendelea kuchukua nafasi katika jamii, haoni sababu ya kutengua au kupunguza adhabu kwenye rufani hiyo namba 115/2017.

Kwa maana hiyo, alisema mleta maombi ataendelea kuitumikia adhabu ya kifungo cha maisha jela kwa kumwingilia kimwili mwanamke aliyekuwa mkewe, Ezinara Wilson (46).



# Hemed aahidi kuzipa ushirikiano taasisi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema Serikali ya Zanzibar itaendelea kutoa ushirikiano kwa taasisi na mashirika yote yenye nia kushirkiana na Serikali katika kuwaletea huduma wananchi wake.

Hemed alieleza hayo jana wakati akizungumza na viongozi wa Shirika la Kimataifa la Maendeleo Duniani, linalosaidia kutoa huduma za kuwafikia watu wenye Ulemavu Duniani (CBM) waliofika ofisini kwake Vuga jijini Zanzibar.

Alisema Zanzibar kuna uhitaji mkubwa wa huduma mbalimbali kwa wananchi wake, hivyo ujio wa Shirika hilo kutasaidia kwa kiasi kikubwa kuwafikia wananchi, na kuwapatia huduma ikiwemo matibabu ya macho sambamba na kuwasaidia watu wenye ulemavu.

Makamu wa Pili wa Rais alieleza kuwa, Serikali haina pingamizi lolotee juu ya utekelezaji wa huduma zinzotolewa na CBM, na ameuagiza uongozi wa Wiara ya Afya Ustawi wa Jamii Wazee Jinsia na Watoto, kuhakikisha mpango huo unaanza haraka utekelezaji wake kwa kutoa huduma kwa jamii.

Naye, Mkurugenzi Mkazi wa CBM, Nesia Mahange, alisema shirika lao limeamua kuunga mkono jitihada za serikali ya Mapinduzi Zanzibar kutokana na uhitaji mkubwa uliopo wa huduma za macho pamoja na masuala mbali mbali ya kijamii yanayohusu mambo ya kimaendeleo.

Mkurugenzi Nesia alisema la CBM lina zaidi ya miaka 50 tangu kuanzishwa kwake na linatoa huduma za rasilimali fedha,utaalamu, kujenga miundombinu, kutoa elimu jumuishi na kusomesha wataalamu kupitia sekta ya Afya ya macho, elimu jumuishi, makaazi pamoja misaada ya huduma za kibinadamu itokanayo na masuala ya maafa.

# Othman ataka chombo kusimamia madampo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar , Othman Masoud Othman, amesema ni muhimu Zanzibar kuwa na chombo rasmi chenye uwezo na mamlaka ya kisheria kusimamia masuala yanayohusu madampo na taka za aina mbalimbali zinazozalishwa kwenye maeneo tofauti ikiwamo hospitalini.

Aliyasema hayo jana ofisini kwake Mjini Zanzibar, katika kikao maalum cha mwendelezo wa tathmini ya ziara yake ya kimazingira ya hivi karibuni, kilichowashirikisha watendaji wa Jiji la Zanzibar, Manispaa, Mamlaka ya Usimamizi Mazingira na wa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ.

Alisema pamoja na serikali kutumia zaidi ya Sh. bilioni 21 kufanya uwekezaji mkubwa wa ujenzi wa miundombinu ya dampo la Kisasa huko Kibele, kutupa taka na kulinda mazingira, lakini halitumiki ipasavyo kutokana na kuwapo changamoto ya rasilimali watu na bajeti ya uendeshaji na hivyo kuelekea kutofikiwa matarajio ya dampo hilo.

Alisema hatua ya kuwa na chombo cha aina hiyo ni muhimu kwa kusaidia Zanzibar kuweka mfumo bora na sahihi zaidi katika hatua za ukusanyaji wa taka, usafirishaji na usimamizi utakaokidhi haja na matarajio kwa hali ya sasa na ya baadae katika utunzaji wa mazingira.

Alieleza kuwa dampo la Kibele lina mfumo bora wa kitaalamu katika kusimiamia na kutenganisha taka za aina mbalimbali pamoja na uwezo wa kuzalisha bidhaa kama vile mbolea, lakini baadhi ya vifaa vilivyopo ambavyo ni vya gharama kubwa havitumiki kwa sababu mbalimbali, jambo linalotishia kutofikiwa matarajio ya kujengwa jaa hilo.

Aidha, alisema dampo la Kibele ni miongoni mwa madampo ya kisasa na limeigharimu serikali kiasi kikubwa cha fedha, lakini iwapo hakutakuwa na chombo chenye jukumu rasmi la usimamizi wa taka, ujenzi huo hautakuwa na maana yoyote katika kuweka usafi na utunzaji wa mazingira.

Othman pia katika kikao hicho aliagiza mamlaka zinazohusika na usimamizi wa janga hilo kuhakikisha wanaweka mipango bora na kutatua kwa haraka baadhi ya changamoto zilizopo ikiwemo uhaba wa rasilimali watu na mafuta ya kuendeshea baadhi ya mitambo ya jaa hilo.

Naye Meneja wa dampo la Kibele, Hassan Mohammed Ali, alisema dampo hilo ni miongoni mwa madampo bora Afrika, lakini linakabiliwa na changamoto nyingi ikiwamo baadhi ya vifaa kutotumika hadi sasa, kutupwa baadhi ya taka hatarishi zikiwemo za hospitali licha ya kwamba kitaalam hazipaswi kutupwa katika eneo hilo kwa vile zinaweza kuleta madhara makubwa kwa binaadamu.

Meya wa Jiji la Zanzibar, Mstahiki Mahmoud Mohammed Mussa, alikiri kwamba taka za hospitali pamoja na kwamba ni hatarishi, lakini zinaendelea kutupwa katika eneo hilo kutokana na vifaa vya kuchomea taka za aina hiyo katika Hosptali ya Mnazi Mmoja kuharibika mara kwa mara.



Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Dk. Juma Malik Akili (wa tatu kushoto), akiongoza uzinduzi wa huduma ya kidijitali ya VodaBima kupitia ushirikiano wa kiutendaji na Shirika la Bima Zanzibar (ZIC) na Kampuni ya Vodacom Tanzania, jijini Zanzibar jana. Wengine ni Kamishna wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Dk. Mussa Juma (kulia), Naibu Kamishna wa TIRA, Khadija Issa Said (kushoto), Mkurugenzi Mkuu wa ZIC, Arafat Haji (wa pili kulia) na Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Biashara M-Pesa, Rashid. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SMZ yapongeza jitihada za ZIC kuboresha huduma

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Ofisi ya Rais (Fedha na Mipango) Dkt. Juma Malik Akili, amepongeza jitihada zinazoendelea kufanywa na Shirika la Bima Zanzibar (ZIC)kwa kuendelea kubuni namna mbalimbali katika kurahisisha upatikanaji wa huduma ya bima kwa wateja wake na jamii kwa ujumla.

Amesema hatua hiyo inakwenda sambamba na nia ya serikali katika kuboresha sekta ya Bima nchini kwa kupanua ushiriki wa wananchi katika shughuli za kibima.

Akizungumza kwenye hafla fupi ya uzinduzi wa huduma ya kidijitali ya VodaBima kupitia ushirikiano wa kiutendaji baina ya ZIC na Kampuni ya Vodacom Tanzania iliyofanyika visiwani Zanzibar jana, Dk. Akili alisema hatua hiyo inadhihirisha nia ya Shirika hilo ya kutoa huduma kwa wananchi wengi zaidi na kuwapatia huduma ya bima karibu zaidi na maeneo yao kulingana na azma ya serikali.

"Kupitia huduma hii ya VodaBima wananchi sasa watapata huduma za kibima kwa ukaribu zaidi kupitia simu zao za mkononi na hivyo kuongeza urahisi katika upatikanaji wa huduma hiyo na kuongeza wigo wa kuwafikia wateja na wanachi kwa ujumla na hivyo kukuza sekta ya bima nchini."

"Na hii ndio sababu nawapongeza sana ZIC kwa juhudi zao za kuendelea kuwafikia wanachi na wateja wao kwa ukaribu na huu ukiwa ni mwendelezo wa jitihada walizozifanya hivi karibuni kwa kuingia kwenye makubaliano ya kiuendaji kama haya na Shirika la Posta Tanzania. Nadiriki kusema hii ni heshima na moja ya mafanikio kwa serikali ya Mapinduzi Zanzibar inayoadhimisha mwaka mmoja tangu Rais Dokta Hussen Ali Mwinyi aingie madarakani." Alisema.

Dk. Akili aliipongeza kampuni ya Vodacom Tanzania kwa ushirikiano huo, huku akiiomba kampuni hiyo kuendelea kujitanua zaidi katika visiwa hivyo ili wananchi waendelee kufaidi zaidi huduma za shirika hilo zikiwemo zile za kibiashara na kijamii kupitia simu za mkononi.

Kwa upande wake Kamishna wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) Dk. Mussa Juma, pamoja na kupongeza taasisi hizo mbili kwa ushirikiano huo kupitia ubunifu, alitoa wito kwa kampuni za bima nchini kuendelea kubuni zaidi huduma mbalimbali za kibima ili kuongeza wigo wa huduma za kibima sambamba na na njia (distribution channels) za kuwafikia wateja wao."Hiki ninachokishuhudia hii leo ni mwanzo mzuri kwasababu tulianza ushirikiano na mabenki kupitia huduma za bancassurance na sasa tunaingia kwenye kampuni za simu na Vodacom wanakuwa wa kwanza kufanikisha hili nawapongeza sana! Pongezi pia kwa ZIC kwa kuchangamkia fursa hii naomba na wengine waendelee kuiga na kubuni namna zaidi ya kuwafikia wananchi kwasababu bado tupo nyuma katika ufikiaji wa huduma za kibima kwa wananchi," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa ZIC, Arafat Haj, alisema mbali na kuunga mkono jitihada za serikali katika kuboresha sekta ya Bima nchini, hatua hiyo ni mwendelezo wa mkakati wa Shirika hilo kusaidia jamii kufikiwa na huduma za bima kwa ukaribu zaidi na kuongeza urahisi wa upatikanaji wa huduma hiyo na kukuza sekta ya bima nchini kwa ujumla.

"Mkakati huu unakuja tukitambua fika kwamba kwasasa ufikiwaji wa huduma ya bima kwa wananchi ni asilimia 30 tu hivyo jitihada zaidi zinahitajika. Tunaamini kupitia huduma hii ya VodaBima inayotumia miundombinu bora ya teknolojia ya M-Pesa na mtandao mpana wa Vodacom ambayo inapatikana katika maduka ya Vodacom nchini kote tunakwenda kuwafikia wateja wetu kwa urahisi zaidi huku pia tukiwahakikishia usalama zaidi katika utoaji wa huduma zetu za kibima.... tunaomba sana watuunge mkono," alisema.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Biashara M-Pesa, Rashid Tulisindo, alisema kupitia huduma hiyo ya VodaBima kampuni hiyo inakusudia kuziba pengo la upatikanaji wa huduma za bima kwa kutoa suluhisho la kidijitali ambalo litapunguza gharama na kuongeza upatikanaji wa bidhaa za Bima.

Alisema VodaBima inatumia miundombinu bora ya teknolojia ya M-Pesa na mtandao mpana wa Vodacom ambayo inapatikana katika maduka Vodacom nchini kote kuhakikisha usalama, urahisi wa upatikanaji wa huduma za bima.

Hafla ya uzinduzi huo ilihudhuliwa na wadau mbalimbali akiwamo Naibu Kamishna wa TIRA, Khadija Issa Said, baadhi ya viongozi waandamizi wa serikali, wafanyakazi wa Shirika la Bima Zanzibar (ZIC) na wafanyakazi wa Kampuni ya Vodacom Tanzania.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

GARI INAUZWA AINA YA VOLKSWAGEN TOUREG YA MWAKA 2004 NAMBA DDV RANGI NYEUSI. INATEMBEA NA IKO KWENYE HALI NZURI SANA. BEI NI TSH. 15,000,000/- PIGA SIMU NAMBA 0762 810 451.

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

## KUPOTEA KWA VYETI



116554402

**HADIJA GODFREY** anatangaza kupotelewa na vyeti ,cha kidato cha nne chenye index namba P0301-0480 kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule/kituo cha AIRWING JWTZ CENTRE(tanga) MWAKA 2014,na CERTIFICATE ya chuo cha TANZANIA PUBLIC SERVICE COLLEGE yenye registration namba DSS.03/17/TG.124 mwaka 2018,na cheti cha diploma ya chuo cha TANZANIA PUBLIC SERVICE COLLEGE chenye namba DSS.03/17/TG.124 mwaka 2019,yeyote atakayeviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa MUH/RB/2939/2021

## KUPOTEA KWA VYETI



**BRIAN AMAN KISAMO** anatangaza kupotelewa na vyeti vifuatavyo,cha kidato cha nne chenye index namba S2376-0198 kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia **MUGABE SECONDARY** mwaka 2013 na cheti cha kidato cha sita chenye index namba S0347-0883 kilichotolewa na baraza lamitihani kupitia **TAMBAZA SECONDARY** mwaka 2016,yeyote atakayeviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **DAR/MBU/RB/526154/2021**

## KUPOTEA KWA VYETI



116554002

MUJIBU MAJALIWA ABUNWAS anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.2306/0033 kilichotoklewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya BUSANDA mwaka 2018 na result slip ya kidato cha sita yenye index namba S.0153/0541 kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya SONGEA BOYS mwaka 2021,yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa MBE/MBE/RB/522698/2021

## KUPOTEA KWA VYETI



116554202

ELVINUS PATHIENCE anatangaza kupotelewa na vyeti,cha kidato cha nne chenye index namba S0405-0070 kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary BIHARAMULO mwaka 2012 na cheti cha kidato cha sita chenye index namba S0612-0515 kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya sekondary ya KAGANGO mwaka 2015,yeyote atakayeviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa DAR/KIG/RB/880430/2020

## KUPOTEA KWA CHETI



116554302

**UMMY LIUTE NGONDAE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1045/0088** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya **DAR ES SALAAM SECONDARY** mwaka 2018,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **CONTROL NAMBA 9910830771718**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

KING LION natangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili MC 888 BEH, chasis namba TBPK8B8G2K01674,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa MKB/RB/3215/2021


## KUPOTEA KWA CHETI



116554502

DAVIS MENYIASUMBA anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0363/0084 kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya sekondaryya MWADUI mwaka 2018,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochiote cha polisi Polisi taarifa DAR/CHU/RB/526939/2021

## KUPOTEA KWA CHETI



116553802

**ANDREA J MTISHIRE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S 2257/0086** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya MJI MPYA mwaka 2018, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **KIL/MOS/RB/257355/2021**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

EVA IDDI MSANGI, Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki Yenye namba za usajili MC 632 BAU . Engine namba KL157FM13J19607 namba Chassis namba LTBPK82B9D1C19559 Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .
Polisi Taafifa : KIL/MOS/RB/523002/2021

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

FRANK ANDREW HAULE anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya TVS KING yenye namba za usajili MC 335 BPT,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa MKB/RB/226/2021

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**REHEMA IBRAHIMU SHABHAY** anatangaza kupotelewa na kadi ya bajaji yenye namba za usajili **MC T.346 BNX** ,CHASSIS NO: **MD2 AAAA ZZSWJ54869,** ENGINE **NO: AAMBSJO4055,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi, Polisi taarifa
**TAN/RB/521707/2021**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya njombe
Kituo cha njombe mjini
Usimamizi wa mirathi na 99/2021
Katika shauri la mirathi ya marehemu.....................
CHARLES MWANGENI wa KWIVAHA
Katika shauri la maombi ya kumteua msimamizi yaliyoletwa na mwombaji...................................
ANGELA CHARLES MWANGENI

TANGAZO KWA UMMA
(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama ya mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote au maslahio yoyote na mirthi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 17 mwezi 11 mwaka 2021.kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo,mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa kabla au mpaka ytarehe tajwa hapo juu.zingatia.endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
Marehemu hakuacha wosia
Imetolewa leo tarehe 03/11/2021



## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NUHU MARSHAL SANGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA VEROSSA** namba za usajili **T 306 BJU** Chassis No. **GX1106027535,** Engine No.**1GEAA7537.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi **DOM /TR/RB/2643/2018.**

## TAARIFA YA KUFUNGA KAMPUNI

**H-DAUGHTERS MICROFINANCE COMPANY LIMITED** tunapenda kuutarifu umma kuwa katika kikao cha bodi ya wakurugenzi kilichofanyika tarehe 29/10/2021 kiliazimia kufunga kampuni ya **H-DAUGHTERS MICROFINANCE COMPANY LIMITED** yenye usajili **No.136864157** kuanzia tarehe **29/10/2021,** kwa mawasiliano/madai wasiliana na **Tell:0764306503** au barua pepe **felicianjb@gmail.com**

## TAARIFA KWA UMMA

**TAFFA** INATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHA USAJILI NAMBA **SO.6140** KILICHOTOLEWA NA MSAJILI WA JUMUIYA. TAARIFA IMETOLEWA KATIKA KITUO CHA POLISI KATI NA KUPEWA KUMBU KUMBU NA. **DAR/CEN/RB/491913/2021**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SELEMANI AMIRI ABDALA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **NISSAN CARACAN** yenye namba za usajili **T.201 CKQ , CHASSIS NO: GWMGE24007090, ENGINE NO: QD32083698,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **TAN/RB/521710/2021**

**OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Sita wahukumiwa kunyongwa hadi kufa kwa mauaji kukusudia

**Na Joctan Ngelly,**

MAHAKAMA Kuu Tanzania Kanda ya Mwanza iliyoketi Geita imewahukumu watu sita kunyongwa hadi kufa kwa makosa ya mauaji ya kukusudia.

Waliohukumiwa ni Sabasaba Enos, Manoni Isheli, Elias Danieli, Musa Paulo, Rubeni Kakinda na Method Cherehani.

Hukumu hiyo imetolewa jana na Jaji wa Mahakama hiyo, Fredrick Manyanda, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kuwa washtakiwa hao walitenda makosa hayo ya mauaji ya kukusudia.

Manyanda alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya washtakiwa hao ili iwe fundisho kwao na kwa watu wengine wenye tabia ya kuua watu kwa makusudi.

Alisema upande wa mashtaka ulipeleka mahakamani mashahidi tofauti kwenye kesi mbalimbali na vielelezo ambavyo vilithibitisha washtakiwa waliua watu maeneo tofuati kwa makusudi.

Upande wa mashtaka ulikuwa ukiongozwa na Mawakili wa Serikali na kwa kesi tofauti na katika kesi hizo upande wa utetezi wa washtakiwa ulikuwa ukiongozwa na mawakili wa kujitegemea.

Jaji huyo alimhukumu Enos kunyongwa hadi kufa kwa makosa mawili ya kumuua kwa kukusudia Joseph Kubona, ambaye ni baba yake mdogo pamoja na Lucia Mpongoni ambaye ni mama yake mdogo.

Pia, alimhukumu Isheli kunyongwa hadi kufa kwa kosa la kumuua kwa kukusudia mama yake mzazi, Njombile Manoni.

Aliwahukumu Elias Danieli na Musa Paulo, kunyongwa hadi kufa kwa kosa la kumuua kwa kukusudia baba yao mzazi, Danieli Kaembe.

Washtakiwa Rubeni Kakinda na Method Cherehani wamehukumiwa kunyongwa hadi kufa kwa kosa la kumuua kwa makusudi Tabu Selemani.

Jaji Manyanda alisema katika kesi hizo mahakama hiyo inawaachia huru watu watatu kwa sababu upande wa mashtaka umeshindwa kuthibitisha mashtaka yao.

Aliwataja waliyoachiwa huru kuwa ni Charles Danieli ambaye alikuwa ameshtakiwa kwa kosa la kumuua kwa kukusudia baba yake mzazi Daniel Kaembe, Sadick Kabale ambaye alikuwa ameshtakiwa kwa kosa la kumuua kwa kukusudia Tabu Selemani na Emmanueli Thobias ambaye alikuwa ameshtakiwa kwa kosa la kumuua Shangazi yake Mary Mashakala.

# Mkakati waja kukabili uhaba mafuta ya kula

**Na Gerald Kitabu**

WIZARA ya kilimo imeweka mikakati ya kuhakikisha uhaba wa mafuta ya kula unamalizika kwa kuzalisha na kusambaza mbegu bora za mazao yanayozalisha mafuta kwa wingi kama alizeti, michikichi, nazi, ufuta, na karanga.

Akifungua kongamano linalojadili sera za namna Tanzania inavyoweza kujitosheleza kwa mafuta ya kula nchini jana jijini Dar es Salaam, Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, alitaja mikakati mingine kuwa ni pamoja na kuboresha shughuli za ugani na bajeti ya shughuli za ugani na utafiti.

Alisema kwa sasa nchi zinazalisha kiasi cha tani 290 za mafuta ya kula nchini, kiasi kikubwa kilichobaki kinaagizwa kutoka nje ya nchi kwa gharama ya Sh. bilioni 475 kwa mwaka.

"Hiki ni kiasi kikubwa sana cha fedha ambacho tukiweza kuokoa kinaweza kusaidia katika kuchangia uchumi wa ndani na kutengeneza ajira zaidi kwa vijana," alisema.

Alisema nchi inazalisha wastani wa asilimia 45 tu, huku ajira nyingi zikienda nje kutokana na kuagiza mafuta ya kula ambayo yanagharimu takribani nusu trilioni. Kwa miaka mitatu tunakuwa tumepeleka nje zaidi ya fedha tulizokopa hivi karibuni IMF, ambazo ni Sh. trilioni 1.3. Alisema ukiona fedha hizo za IMF zinavyotoa huduma za jamii kama kujenga shule shule, vituo vya afya ,nk, utaona jinsi ilivyo bora kutumia fedha zinazokwenda nje kutoa huduma zaidi katika sekta ya kilimo na kutengeneza ajira nchini.

Akizungumzia uzalishaji wa mazao ya muda mfupi kama alizeti, waziri Mkenda alisema kwa sasa mkulima wa kawaida anapata wastani wa tani 0.7 kwa ekari wakati akitumia mbegu bora na kilimo cha kisasa anaweza kupata hadi tani 4.0 kwa ekari moja.

Aliongeza kuwa serikali ina mpango wa kununua pikipiki 2,000 kwa ajili ya maofisa ugani, simu janja na vifaa vya kupimia udongo.

Kwa Afrika Masharki, Tanzania ndo inaongoza kwa uzalishaji wa mafuta ya kula ikifuatiwa na Uganda, huku Ukraine kiongoza ulimwenguni.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Chama cha Wazalisha Mafuta ya kula nchini (TASUPA), Ringo Iringo, alisema kuwa viwanda vingi vinafanya kazi kwa muda mfupi tu malighafi zinaisha kutokana na uzalishaji mdogo.

"Uzalishaji ni mdogo sana. Wakulima wanazalisha tani 352, 908 wakati mahitaji ni zaidi ya tani 1,716,000 kwa mwaka.

Kwa mujibu wa Iringo, Tanzania ina viwanda 775 kuanzia vidogo kabisa, vya kati na vikubwa.

Alishauri serikali kuongeza mashamba kufikia hekari milioni 2.1 hasa kwa wakulima wakubwa ili waweze kuzalisha kwa tija kukidhi mahitaji ya viwanda.

Naye Mratibu wa Kitaifa wa Mazao ya Mafuta ya kula kutoka Taasi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (Tari), Joseph Nzunda alisema kuwa inawezekana kabisa Tanzania kujitosheleza kwa mafuta ya kula kutokana na ardhi kubwa na teknolojia za kisasa za uzalishaji wa mafuta ya kula.

Alisema TARI imejipanga vyema kuongeza uzalishaji kwenye mbegu zote za mafuta ya kula ikiwamo Alizeti, Michikichi, Ufuta na Karanga

Kongamano hilo limeandaliwa na wizara ya fedha na Mipango kwa kushirikiana na Umoja wa Ulaya-EU.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO
BODI YA PAMBA TANZANIA

TAARIFA KWA UMMA

KUSUDIO LA KUUZA KWA MNADA MALI ZA KAMPUNI YA Wi AFRICA (T) LIMITED

Bodi ya Pamba Tanzania inautaarifu umma kuwa Kampuni ya Wi Africa Tanzania Limited ambayo ni mpangaji katika mabohari ya Bodi ya Pamba Tanzania yaliyoko Kurasini Dar es Salaam kwa zaidi ya miaka mitatu. Tangu katikati ya mwaka 2019 wamiliki wa Kampuni hii wameshindwa kulipa kodi ya pango na hawajaonekana ofisini wala kushughulika na mali zilizoko katika mabohari waliyopanga.

Bodi ya Pamba Tanzania imefanya jitihada mbalimbali za kuwatafuta wamiliki wa Kapuni ya Wi Africa Tanzania Limited bila mafanikio.

Kutokana hali hiyo Bodi ya Pamba Tanzania inawataarifu wamiliki wa Kampuni ya Wi Africa Tanzania Limited kujitokeza kwa ajili ya kulipa deni la pango wanalodaiwa ndani ya siku saba (7) kuanzia tarehe ya tangazo hili. Wasipojitokeza mali zilizoko katika mabohari zitauzwa kwa mnada kwa mujibu wa sheria ili kufidia deni la pango ambalo kampuni hii inadaiwa.

Limetolewa na;
BODI YA PAMBA TANZANIA,
S. L. P. 61
MWANZA

Jengo la Pamba, Barabara ya Mkoa, S.L.P. 61, Mwanza. Simu: +255 28 2500528,
Baruapepe: info@tcb.go.tz; tovuti: www.tcb.go.tz1


# RC awa mbogo bei kubwa vifaa ujenzi

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, amepiga marufuku wafanyabiashara mkoani hapa kupandisha bei holela ya vifaa vya ujenzi hasa katika kipindi cha ujenzi wa vyumba vya madarasa.

Alipiga marufuku hiyo jana wakati akipokea taarifa ya ujenzi wa mindombinu katika Shule ya Sekondari Kishapu, ikiwamo ujenzi wa vyumba vya madarasa na kubainishwa kuwa changamoto kubwa ambayo inawakabii ni kupanda kwa bei ya vifaa vya ujenzi.

Alisema katika Mkoa wa Shinyanga, hataki kusikia mfanyabiashara yeyote kapandisha bei ya vifaa vya ujenzi ikiwamo saruji na kutaka wauze kwa bei ya kawaida na wakiendelea kuuza bei juu, atawashughulikia.

"Nakuagiza Kamanda wa Polisi Mkoa, mfanyabiashara yeyote ambaye atabainika kupandisha bei ya vifaa vya ujenzi mchukulieni hatua. Hatutaki mtu yeyote atukwamishe kwenye ujenzi huu wa vyumba vya madarasa," alisema Mjema.

"Unapopandisha bei ya vifaa vya ujenzi, ina maana Rais atuongezee tena fedha. Hili sitakubaliana nalo, lazima bei iwe ya kawaida na si kutumia fursa kwenye ujenzi wa vyumba vya madarasa," aliongeza.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi ya Shule hiyo, Maburugi Samweli, akisoma taarifa, alisema changamoto kubwa ambayo inawakabili kwa sasa katika ujenzi huo, ni upandaji wa bei ya vifaa vya ujenzi hasa saruji, hivyo kufanya ujenzi kusuasua.

**"Unapopandisha bei ya vifaa vya ujenzi, ina maana Rais atuongezee tena fedha. Hili sitakubaliana nalo, lazima bei iwe ya kawaida na si kutumia fursa kwenye ujenzi wa vyumba vya madarasa," aliongeza**

# MAKAME AMWOMBA RADHI KAPOMBE KWA RAFU MBAYA

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya juzi kuonekana akipinga maamuzi ya mwamuzi Nassoro Mwichui kutoka Pwani baada ya kumwonyesha kadi nyekundu, Kiungo wa Namungu FC, Abdulaziz Makame, ameonyesha uungwana baada ya kutafakari na kuona ipo haja ya kumwomba msamaha beki wa Simba, Shomari Kapombe, kutokana mchezo usio wa kiungwana aliomchezea.

Kupitia mtandao wake wa kijamii wa Instagram, Makame amemwomba radhi Kapombe kwa kumchezea mchezo usio wa kiungwana katika dakika ya 50, uliomfanya mwamuzi, Mwichui kumtoa nje kwa kadi nyekundu, hivyo kuigharimu timu yake kwa kubaki pungufu uwanjani na hatimaye kufungwa bao 1-0 kwenye mechi hiyo ya Ligi Kuu iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi.

Makame amesema haikuwa dhamira yake kucheza rafu hiyo bali lengo lake lilikuwa kutekeleza majukumu yake uwanjani kama mchezaji.

"Napenda kuchukua fursa hii kuwaomba radhi Watanzania na wapenda soka wote, kipekee zaidi nimwombe radhi mchezaji wa Simba, Shomari Kapombe kwa mchezo ambao sio wakiungwana, haikuwa dhamira yangu kumchezea rafu ni katika kutimiza wajibu wangu uwanjani kama mchezaji.

"Mpira ni mchezo wa amani na tunashauriwa kucheza 'Fair', timu yangu ya Namungo chini ya kocha wangu, Morocco [Hemed] naomba radhi kwa kuigharimu timu yangu kucheza pungufu. Naahidi kuzidisha umakini katika mechi zinazofuata," aliandika kupitia ukurasa wake wa Instagram.

Kumekuwa na matumizi makubwa ya nguvu yanayochangia wachezaji kutoonyesha mchezo wa kiungwana uwanjani hususan zinapocheza dhidi ya bingwa huyo mtetezi, Simba.

Kwa kuthibitisha hilo, kati ya michezo mitano ambayo Simba imecheza hadi sasa, mechi nne wachezaji wa timu pinzani wameonyeshwa kadi nyekundu.

Katika mechi dhidi ya Dodoma Jiji FC dhidi ya Simba iliyopigwa Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma, Anuary Jabir alitolewa kwa kadi nyekundu baada ya kumchezea rafu mbaya beki Kennedy Juma hadi kushindwa kuendelea na mchezo huo uliomalizika kwa Simba kushinda bao 1-0.

Kadhalika, wakati Simba ikishinda bao 1-0 dhidi ya Polisi Tanzania katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Juma Ramadhani naye alionyeshwa kadi nyekundu kwa rafu mbaya dhidi ya winga Bernard Morrison huku Benedictor Jacob Mwamlangwa wa Coastal Union naye akikumbana na adhabu hiyo, kabla ya Makame kwa Kapombe juzi.

Katika mechi hiyo ya Ligi Kuu Bara dhdi ya Namungo, Simba ilishinda bao 1-0, shukrani kwa mtokea benchi Meddie Kagere aliyeifungia timu yake dakika za majeruhi.

Kwa matokeo hayo, Simba imepanda hadi nafasi ya pili ikiwa na pointi nne nyuma ya vinara Yanga wenye alama 15 huku Namungo ikisalia na pointi zake tano hadi wakati huu timu zote zikiwa zimeshuka dimbani mara tano.

## Morocco atoa sababu kipigo Simba

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Namungo, Hemed Suleiman 'Morocco', amesema kukosekana kwa umakini mwishoni mwa mchezo, ndiko kulikosababisha kupoteza mechi hiyo ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Simba juzi usiku kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mechi hiyo, timu yake ikipoteza kwa bao 1-0 lililofungwa dakika ya nne ya nyongeza na Mnyarwanda, Meddie Kagere, alisema ni mechi ambayo walihitaji ushindi au sare, lakini wakapoteza dakika za mwisho kutokana na wachezaji wake kushindwa kuwa makini mwishoni wakati mechi ikiwa karibu kumalizika.

"Tumepoteza mechi na tunasikitika sana, lakini kwa sasa hata tuseme nini ndiyo imeshaisha hivyo, tumefungwa, niwapongeze Simba kwa kutumia vema mwanya wa kushuka kwa umakini wetu kwenye dakika za mwisho," alisema Morocco, kiungo wa za zamani wa Coastal Union.

Alisema waliingia na mpango mkakati wa kuwazuia Simba wasifanye chochote kwa dakika 25 mpaka 30 kwani walijua wataingia kwa kasi kutafuta bao na waliweza kufanya hivyo, na kipindi cha pili waliingia na mfumo mwingine.

"Tulibadilisha mfumo kipindi cha pili, sasa tulitaka kutafuta bao, lakini kwa bahati mbaya mchezaji wetu mmoja alipata kadi nyekundu, ikatuathiri, lakini niwapongeze wachezaji wangu waliweza kupambana hadi mwisho wa mchezo, licha ya kuruhusu bao mwishoni," alisema.

Kwa matokeo hayo, Namungo imesalia na pointi zake tano kwa mechi tano ilizocheza, huku Simba ikikwea hadi nafasi ya pili kwa pointi 11, nyuma ya vinara Yanga wenye alama 15.

**IKO HIVI...**




Kiungo wa Simba, Ibrahim Ajibu (katikati), akichezewa madhambi na mchezaji wa Namungo FC, kabla ya kupiga faulo hiyo kwenda kwa Muhamed Hussein 'Tshabalala' aliyepiga krosi na kuzamishwa nyavuni kwa kichwa na Meddie Kagere katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi. **MPIGAPICHA WETU**

## KMC kutafuta dawa ya kujinasua mkiani

**Na Saada Akida**

BAADA ya kushuhudia timu yake ikiburuza mkia ikiwa na pointi mbili kwenye msimamo wa Ligi Kuu baada ya michezo mitano hadi wakati huu timu zikienda mapumzikoni kupisha Kalenda ya Fifa, Kocha wa KMC FC, Habib Kondo, amesema wachezaji wake hawatakuwa na mapumziko hayo.

KMC FC inaburuza mkia ikiwa na pointi mbili kama ilivyo kwa Mtibwa Sugar, Geita Gold na Tanzania Prisons, ambazo zinaizidi kwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kondo alisema kulingana na ugumu wa ligi msimu huu hataweza kuwapa mapumziko wachezaji wake kwani anahitaji kutumia vizuri wiki mbili za Kalenda ya Fifa kukisuka kikosi chake.

**"Tumepoteza mechi tatu na sare mbili, kwa matokeo haya inaonyesha kwamba tuna mapungufu katika kikosi chetu, hiki kipindi cha wiki mbili hatutakuwa na mapumziko zaidi ya kuendelea kubaki kambini kwa ajili ya kufanyia kazi mapungufu yetu," alisema kocha huyo.**

Alisema msimu huu umekuwa mgumu hivyo anataka kuhakikisha anatumia vema mapumziko hayo kwa sababu kila timu imejipanga kufanya vizuri.

"Baada ya wiki hizi mbili, tunakuja kucheza na Azam FC, mechi ngumu sana hiyo, muda huu tunatakiwa kupambana kufanyia kazi mapungufu yetu na kujiimarisha kwa ajili ya kwenda kutafuta pointi muhimu katika mchezo huo na inayoendelea," alisema Kondo.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### COUTINHO KUUZWA NEWCASTLE

NEWCASTLE inatarajiwa kumsajili mchezaji wa zamani wa Liverpool, kiungo wa kati Philippe Coutinho, huku Barcelona wakitamani kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29. **(Sport)**

### TCHOUAMENI AFUATILIWA

KLABU ya Manchester United inapanga kumfuatilia kiungo wa kati wa Monaco, Aurelien Tchouameni mwenye umri wa miaka 21, huku wakiongeza kasi ya kutafuta mbadala wa nyota wa Ufaransa, Paul Pogba mwenye miaka 28. **(Football Insider)**

### MBAPPE ATAKA OLIMPIKI

MSHAMBULIAJI wa Paris St-Germain, Kylian Mbappe anaweza kutaka kipengele cha Olimpiki kiingizwe katika mkataba wowote unaowezekana na Real Madrid baada ya mchezaji huyo mwenye miaka 22, kueleza hadharani nia yake ya kuiwakilisha Ufaransa kwenye michezo hiyo itakayofanyika jijini Paris mwaka 2024. **(AS)**

### CAVANI ATAKIWA PALMEIRAS

KLABU ya Palmeiras ya Brazil inapenda kumsajili mshambuliaji wa Manchester United, Edinson Cavani mwenye umri wa miaka 34, pale mkataba wa mchezaji huyo wa Uruguay utakapokwisha majira ya joto yajayo. **(Daily Express)**

### RODGERS AMULIKWA CITY

KLABU ya Manchester City wamemwambia kocha wa Leicester, Brendan Rodgers mwenye umri wa miaka 48, kuwa wangependa achukue mikoba ya Pep Guardiola mara raia huyo wa Hispania mwenye miaka 50 atakapoachana na mabingwa hao wa Ligi Kuu England. **(The Transfer Podcast via Leicester Mercury)**

### VLAHOVIC ANUKIA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inaongoza kinyang'anyiro cha kumnasa mshambuliaji wa Fiorentina, Dusan Vlahovic mwenye umri wa miaka 21, huku raia huyo wa Serbia akiwa tayari kuhamia Ligi Kuu England. **(La Nazione)**

### DEMBELE KUBAKI BARCA

BARCELONA ina matumaini ya kumshikilia winga wa Ufaransa, Ousmane Dembele mwenye umri wa miaka 24 na kumpa mkataba mpya wa miaka mitatu ifikapo mwishoni mwa Novemba. Dembele, ambaye mkataba wake wa sasa unaisha msimu ujao wa majira ya joto, inasemekana amekubali kukatwa mshahara. **(Mundo Deportivo)**

### BABA HUYO EVERTON

EVERTON wanafikiria kumnunua kiungo wa kati wa Real Mallorca na Ghana, Iddrisu Baba mwenye umri wa miaka 25, Januari mwakani. **(Fichajes via Daily Mail)**

### NDOMBELE ATAKIWA BARCA

BARCELONA watamchukua kiungo wa kati wa Tottenham Hotspur mwenye umri wa miaka 24, Tanguy Ndombele Januari, lakini wanaweza tu kumudu mkataba wa mkopo kwa Mfaransa huyo. **(Sport)**

### EMERY AIKATAA NEWCASTLE

KOCHA wa Villrreal, Unai Emery mwenye umri wa miaka 50, ametupilia mbali ofa ya Newcastle kwa sababu klabu hiyo imetaka kiwapo kipengele kwenye mkataba wake kitakachowaruhusu kumtimua ikiwa watashuka daraja mwishoni mwa msimu. **(Daily Mirror)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA ATOA SIRI UGUMU MATAJI CITY, BAYERN, BARCA

●●● Yote niliyoshinda kabla kwa sababu nilikuwa kwenye klabu kubwa, lakini ukiwa hapa City presha ni...

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola amesema anaridhishwa na mafanikio anayoyapata akiwa na Manchester City kwa sababu "hakuna anayewasaidia" wao kama ilivyo kwa klabu nyingine kubwa.

City walipaa kileleni mwa kundi A kwenye Ligi ya mabingwa Ulaya baada ya kushinda mabao 4-1 dhidi ya Club Brugge pale dimba la Etihad Jumatano, ingawa walikabiliwa na wakati mgumu kipindi cha kwanza kwa John Stones kujifunga na kusawazisha lile la ufunguzi la Phil Foden la dakika ya 15.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu England walionekana kuimarika zaidi baada ya kipindi cha kwanza na walipata ushindi muhimu kwa mabao kutoka kwa Riyad Mahrez, Raheem Sterling na Gabriel Jesus.

Hiyo ilitosha kuwapeleka City kileleni kwani Paris Saint-Germain walilazimishwa sare ya kufungana mabao 2-2 na RB Leipzig baada ya penalti ya Dominik Szoboszlai.

Wakati ilionekana kama Leipzig waliwasaidia City kwa kupata sare, Guardiola aliiambia BT Sport: "Tunasaidiana wenyewe. Tulichokifanya kwa miaka yote... ilikuwa ni juhudi zetu wenyewe, kama ukiwa hapa Manchester City, unaweza kukubali kwamba hauna mtu anayekusaidia. Hakuna hata mmoja.

"Kila kitu tulichofanya, tumefanya wenyewe. Wakati kwenye klabu kubwa ni tofauti. Hapa hapana, hapana. Tukishinda tumepambana wenyewe tu."

Aliendelea, huku akitabasamu: "Mataji yote niliyoshinda kabla kwa sababu nilikuwa kwenye klabu kubwa.

"Lakini kwa uhakika kabisa ukiwa hapa (City) presha ni kubwa sana. Hapa lazima upambane kushinda kila kitu mwenyewe."









# ANCELOTTI AOMBA RADHI KWA HAZARD

**MADRID, Hispania**

KOCHA Mkuu wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, anaelewa namna Eden Hazard alivyochanganyikiwa na ameomba radhi kwa kumuacha benchi Jumatano wakati wakishinda mabao 2-1 dhidi ya Shakhtar Donetsk kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Hazard mwenye umri wa miaka 30, amecheza mechi moja tu kwa Madrid kati ya nne za Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu, akianza katika kichapo cha 2-1 kutoka kwa Sheriff.

Aidha, mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji, Hazard ameanza katika mechi tano na kucheza mara tano kwenye mashindano yote, akifikisha dakika 409 msimu huu, huku Vinicius Junior akiongoza safu ya ushambuliaji kutokea winga ya kushoto.

Hali hiyo imeibua uvumi kwamba, Hazard ambaye aliweka rekodi ya usajili hapo 'Los Blancos' kutoka Chelsea mwaka 2019, anaweza kuondoka Madrid, Januari.

Ancelotti alimuacha nje kwenye mchezo wa Jumatano huku akifanya mabadiliko mawili tu dhidi ya Shakhtar.

"Kuchanganyikiwa ni kawaida. Naamini jambo kama hilo ni la kawaida kwa mchezaji yoyote," alisema Ancelotti akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Naelewa vizuri sana hali inavyokuwa kwa mchezaji ambaye hapati nafasi ya kucheza, hilo ni kawaida tu.

"Pia naelewa namna anavyohisi mchezaji anayefanya mazoezi kwa dakika 40, lakini hapati nafasi ya kucheza. Samahani sana kwake, niliwaambia wachezaji: Samahani, lakini sikufanya mabadiliko yoyote."

# Pochettino hakieleweki PSG



**PARIS, Ufaransa**

KOCHA wa Paris Saint-Germain, Mauricio Pochettino, aliachwa kachanganyikiwa baada ya kikosi chake kuruhusu penalti ya dakika ya mwisho na kulazimishwa sare ya mabao 2-2 na RB Leipzig na kushindwa kupaa kileleni mwa msimamo wa Kundi A kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, Jumatano.

PSG walianza kuwa nyuma kwa bao la mchezaji wao wa zamani, Christopher Nkunku akifunga kwa krosi ya Andre Silva, na wangeweza kufungwa tena dakika 12 kama golikipa Gianluigi Donnarumma asingeokoa penalti ya Danilo.

Georginio Wijnaldum alifunga mabao yake ya kwanza mawili kwa PSG tangu alipojiunga akitokea Liverpool na kuifanya timu yake kuongoza, lakini vijana hao wa Pochettino wakajikuta wakipoteza pointi mbili.

Presnel Kimpembe alitoa penalti na Dominik Szoboszlai akaifunga dakika ya 92 ya mchezo huo.

"Tumeona ukiikabili timu inayocheza vizuri unavyotengeneza matatizo," alisema Pochettino akiambia RMC Sport.

"Ni makosa yetu tulishindwa kutumia vizuri nafasi tulizozipata. Ni kweli kwamba hatukuanza vizuri.

"Na kipindi cha pili, tulitawala mchezo vizuri sana. Takwimu zinatuonyesha kwamba, tulikuwa na nafasi nzuri ya kufunga."

## HABARI MICHEZO


2,668,240

JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 06/11/21 | 18:00 | Crystal Palace vs Wolverhampton | 2.42 | 3.14 | 3.04 |
| 02. 06/11/21 | 18:00 | Blackburn vs Sheffield Utd | 2.32 | 3.29 | 2.89 |
| 03. 06/11/21 | 18:00 | Luton Town vs Stoke City | 2.27 | 3.21 | 3.06 |
| 04. 06/11/21 | 18:00 | Barnsley vs Hull City | 2.44 | 3.09 | 2.89 |
| 05. 06/11/21 | 20:30 | Alaves vs Levante | 2.55 | 3.05 | 2.95 |
| 06. 06/11/21 | 20:30 | Blackpool vs QPR | 2.44 | 3.28 | 2.74 |
| 07. 07/11/21 | 17:00 | Everton vs Tottenham | 2.65 | 3.15 | 2.75 |
| 08. 07/11/21 | 17:00 | Nantes vs Strasbourg | 2.38 | 3.23 | 2.98 |
| 09. 07/11/21 | 17:00 | Leeds vs Leicester | 2.85 | 3.45 | 2.39 |
| 10. 07/11/21 | 17:00 | Udinese vs Sassuolo | 2.47 | 3.44 | 2.75 |
| 11. 07/11/21 | 20:30 | Osasuna vs Real Sociedad | 2.94 | 3.24 | 2.43 |
| 12. 07/11/21 | 22:45 | Rennes vs Lyon | 2.89 | 3.48 | 2.32 |
| 13. 07/11/21 | 23:00 | Betis vs Sevilla FC | 2.80 | 3.21 | 2.55 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 05 - NOVEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2319 | Dinamo Moscow Youth vs Ural Youth | 1.25 | 5.59 | 8.10 |
| 15:00 | 1268 | Southampton U23 vs Newcastle U23 | 2.36 | 3.70 | 2.75 |
| 15:00 | 2035 | FK Imt Novi Beograd vs Backa Palanka | 1.74 | 3.13 | 4.82 |
| 16:00 | 4176 | NK Sesvete vs Opatija | 2.01 | 3.37 | 3.28 |
| 17:00 | 2579 | Pyunik Yerevan vs Artsakh | 2.07 | 3.27 | 3.22 |
| 18:15 | 5528 | Lokomotive Sofia vs Beroe | 3.22 | 3.22 | 2.09 |
| 19:00 | 2710 | Apollon Limassol vs Doxa Katokopia | 1.43 | 4.55 | 6.73 |
| 19:00 | 4639 | AS Trencin vs Zemplin Michalovce | 1.59 | 3.96 | 4.54 |
| 20:00 | 2310 | Gaziantep BB vs Kasimpasa | 2.18 | 3.40 | 3.11 |
| 20:00 | 2829 | Istanbulspor vs Menemen Bld | 1.52 | 4.03 | 5.18 |
| 20:00 | 5161 | Slaven Belupo vs HNK Gorica | 2.98 | 3.32 | 2.16 |
| 20:00 | 5731 | Caykur Rizespor vs Alanyaspor | 3.50 | 3.50 | 1.99 |
| 20:00 | 5938 | Novi Pazar vs Backa Topola | 3.18 | 3.18 | 2.13 |
| 20:30 | 3089 | Oleksandria vs FC Metalist 1925 | 1.80 | 3.57 | 3.76 |
| 20:30 | 3367 | Nurnberg vs Werder Bremen | 2.80 | 3.29 | 2.39 |
| 20:30 | 3761 | Floridsdorfer AC vs SV Lafnitz | 2.74 | 3.22 | 2.36 |
| 20:30 | 4088 | Kapfenberg vs FC Juniors OO | 2.18 | 3.38 | 2.90 |
| 20:30 | 5583 | Wacker Innsbruck vs SKN St Polten | 1.87 | 3.56 | 3.51 |
| 20:30 | 5929 | Holstein Kiel vs Dynamo Dresden | 1.94 | 3.47 | 3.62 |
| 21:00 | 2515 | Zamalek vs Al Ahly Cairo | 3.06 | 3.01 | 2.41 |
| 21:00 | 4726 | Esbjerg vs Jammerbugt FC | 1.51 | 4.05 | 5.20 |
| 21:00 | 5660 | Viborg FF vs Nordsjalland | 1.94 | 3.73 | 3.44 |
| 21:00 | 5810 | Paeek vs Olympiakos Nicosia | 3.82 | 3.57 | 1.89 |
| 22:00 | 1016 | Gil Vicente vs FC Arouca | 1.98 | 3.25 | 3.80 |
| 22:00 | 1118 | Jong Utrecht vs FC Eindhoven | 2.26 | 3.47 | 2.83 |
| 22:00 | 1659 | Jong PSV vs FC Oss | 2.11 | 3.48 | 3.08 |
| 22:00 | 1988 | VVV Venlo vs Jong Ajax | 2.64 | 3.58 | 2.34 |
| 22:00 | 3221 | Twente vs Heracles Almelo | 2.11 | 3.42 | 3.18 |
| 22:00 | 3287 | Dordrecht vs NAC Breda | 5.06 | 4.47 | 1.51 |
| 22:00 | 4330 | Den Bosch vs De Graafschap | 5.28 | 4.50 | 1.49 |
| 22:00 | 4423 | Helmond Sport vs Roda Kerkrade | 4.68 | 4.00 | 1.61 |
| 22:00 | 4539 | FC Volendam vs Emmen | 2.06 | 3.57 | 3.13 |
| 22:00 | 5936 | Jong AZ Alkmaar vs Maastricht | 2.02 | 3.62 | 3.18 |
| 22:25 | 4941 | Liebherr Gak vs Amstetten | 2.27 | 3.37 | 2.75 |
| 22:30 | 1304 | Mainz vs Monchengladbach | 2.53 | 3.53 | 2.58 |
| 22:30 | 3176 | FC Winterthur vs FC Stade LS Ouchy | 2.33 | 3.33 | 2.70 |
| 22:30 | 3633 | Cosenza vs Reggina | 3.28 | 3.09 | 2.21 |
| 22:30 | 4035 | Neuchatel Xamax vs FC Schaffhausen | 2.09 | 3.51 | 2.98 |
| 22:30 | 5156 | FC Thun vs FC Vaduz | 1.99 | 3.47 | 3.23 |
| 22:45 | 2146 | Waterford Utd vs Shamrock Rovers | 3.23 | 3.32 | 2.04 |
| 22:45 | 2366 | Edinburgh City vs Albion Rovers | 2.04 | 3.43 | 3.14 |
| 22:45 | 2593 | St Patricks vs Sligo Rovers | 2.28 | 3.12 | 2.93 |
| 22:45 | 4207 | OH Leuven vs Oostende | 2.22 | 3.64 | 2.85 |
| 22:45 | 5474 | Empoli vs Genoa | 2.08 | 3.64 | 3.29 |
| 22:55 | 1573 | AFC Sudbury vs Colchester | 7.48 | 5.31 | 1.33 |
| 23:00 | 2358 | Southampton vs Aston Villa | 2.07 | 3.50 | 3.45 |
| 23:00 | 4617 | Finn Harps vs Derry City | 2.66 | 3.14 | 2.47 |
| 23:00 | 4966 | Lens vs Troyes | 1.63 | 3.98 | 4.98 |
| 23:00 | 5020 | Huesca vs Leganes | 2.02 | 3.19 | 3.68 |
| 23:00 | 5052 | Athletic Bilbao vs Cadiz CF | 1.42 | 4.39 | 7.97 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# MOURINHO AISHANGAA SPURS KUMFUKUZA NUNO



**ROME, Italia**

KOCHA wa AS Roma, Jose Mourinho, amehoji uamuzi wa klabu yake ya zamani ya Tottenham Hotspur kumbadilisha Nuno Espirito Santo na Antonio Conte.

Conte raia wa Italia alisaini mkataba wa miezi 18 kuinoa Spurs Jumanne baada ya Nuno kutupiwa virago akiwa ameanza msimu huu kwa kushinda mechi tano na kupoteza tano kati ya 10 za Ligi Kuu England.

Kocha huyo wa zamani wa Wolves kipindi chake cha miezi minne ya kukaa na klabu hiyo ya London Kaskazini kilifikia mwisho Jumatatu baada ya kichapo cha mabao 3-0 kutoka kwa timu ya zamani ya Mourinho, Manchester United.


Wakati alipoulizwa kama Spurs kumchukua Conte kunaweza kuifanya Tottenham kuwa imara, Mourinho aliiambia Sky Sport: "Yeye ni kocha mzuri, lakini Nuno Espirito Santo pia ni kocha mzuri sana ambaye amefanya makubwa kwa miaka minne au mitano pale Wolverhampton.

"Siwezi kusema kwamba, Tottenham wana kocha mzuri hivi sasa, wamefanya hivyo kabla. Wanaye sasa na walifanya hivyo."

Kama ilivyo kwa Mourinho, Conte alifurahia mafanikio muda uliopita kwenye soka la Uingereza akiwa na Chelsea, ambapo aliwaongoza kutwaa taji la Ligi Kuu na FA kwa kipindi cha misimu miwili.

# Xavi ajiandaa kurudi Barcelona

**DOHA, Qatar**



XAVI "kwa uhakika anataka kurudi nyumbani", huku Barcelona ikiwa kwenye mazungumzo na Al Sadd kumfanya yeye kuwa kocha wao mpya.

Makamu wa Kwanza wa Rais wa Barca, Rafael Yuste na Mkurugenzi wa Soka, Mateu Alemany, walihudhuria mchezo wa Al Sadd wakati wakitoka sare ya mabao 3-3 na Al Duhail Jumatano, matokeo ambayo yamemfanya Xavi na kikosi chake kuongoza ligi kwa pointi tatu.

Kiungo huyo wa zamani, ambaye alicheza mechi 767 kwa Barca akiwa mchezaji na kushinda mataji 25 akiwa klabuni hapo, anaongoza katika nafasi ya kupewa kurithi mikoba ya ukocha baada ya kutimuliwa kwa Ronald Koeman wiki iliyopita.

Al Sadd wiki iliyopita ilisisitiza kwamba, Xavi ataendelea kuwa kocha wa klabu hiyo ya Qatari, ambaye amebakiza miaka miwili kwenye mkataba wake, lakini kocha amethibitisha makubaliano kuhusu majaliwa yake yanaweza kufikiwa muda wowote.

"Kwa uhakika nataka kwenda nyumbani. Klabu mbili zipo kwenye mazungumzo na lazima makubaliano yafikiwe.

"Nimehamasika sana, lakini ni suala la muda tu - nina mkataba hapa," alisema Xavi akiiambia Mundo Deportivo.

"Ningependa kurudi nyumbani. Klabu hizi mbili zinatakiwa kukubaliana. Matumaini yangu hilo litafanyika, kwa sababu nina hamu kubwa na nimehamasika sana."

Michezo
Ijumaa Novemba 5, 2021
Nipashe



Guardiola atoa siri ugumu mataji City, Bayern, Barca UKURASA 21

**‘NDONGA’...**




Mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagere, akiunganisha nyavuni kwa ‘ndonga’ [kichwa] mpira wa krosi uliopigwa na Mohamed Hussein ‘Tshabalala’ aliyepokea pasi kutoka kwa Ibrahim Ajibu, kwenye mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Namungo FC iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi, wakishinda 1-0. **MPIGAPICHA WETU**

# AJIBU APATA JIBU SIMBA

●●●Kocha Hitimana amchambua, aomba wiki mbili kutengeneza safu ya mabao huku pia akimtaja Mkude...

**Saada Akida na Faustine Feliciane**

LICHA ya kuingia dakika ya 38 kabla ya mchezo kumalizika, Ibrahim Ajibu, alipata jibu la ushindi Simba wakati ikishinda bao 1-0 juzi dhidi ya Namungo FC kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, jambo ambalo limemuibua Kaimu Kocha Mkuu wa timu hiyo, Thierry Hitimana kwa kuachambua ubora wake.

Katika mechi hiyo bao la Simba lilipatikana baada ya Ajibu kuchezewa madhambi maguu kama 22 kushoto kutoka langoni mwa Namungo, kisha akabeba jukumu la kupiga faulo hiyo kwa kutoa pasi kwa Mohamed Hussein ‘Tshabalala’, aliyepiga krosi iliyosindikizwa nyavuni kwa kichwa na Meddie Kagere dakika za majeruhi.

Hitimana amekunwa na viwango vya nyota wake, hususan Ajibu na Jonas Mkude, akisema iwapo wataendelea kuonyesha ubora walioonyesha kwenye mechi dhidi ya Namungo FC, watajihakikishia namba kikosi cha kwanza.

Tangu kuanza kwa msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara, hiyo ilikuwa mechi ya kwanza kwa Ajibu kucheza huku kwa kiungo mkabaji, Mkude ikiwa ni mchezo wa pili katika michezo mitano ambayo Simba tayari imeshacheza.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Hitimana alisema Ajibu aliingia kipindi cha pili na kuongeza ufundi katika idara ya ushambuliaji kwa kupiga pasi na kuwafungua Namungo ambao muda mwingi walikuwa wanazuia tu.

Alisema Ajibu ni mchezaji mzuri ingawa hajapata nafasi kubwa ya kucheza, lakini kwa kuwa bado wana mechi nyingi za mashindano mbalimbali atazidi kuonekana uwanjani endapo yeye na Mkude wataendelea kuwa na viwango bora kama walichokionyesha katika mchezo huo dhidi ya Namungo.

“Ajibu ni mchezaji mzuri, ana kipaji kikubwa, tulimuingiza baada ya kuona Namungo wanacheza nyuma ili akawafungue, pia tuliona wanacheza faulo na nyota huyo ni mzuri kwenye mipira ya adhabu, tulijua atatusaidia na kweli ametimiza malengo yetu,” alisema Hitimana.

Alisema hiki kipindi cha mapumziko ya wiki mbili kupisha mechi za Kalenda ya Fifa, atakuwa na kazi kubwa ya kukisuka kikosi chake hasa safu yake ya ushambuliaji kuwa makini kwenye nafasi wanazotengeza katika mechi zao.

“Bado tunashida kwenye umaliziaji, tunatengeneza nafasi nyingi, lakini tunashindwa kuzitumia, naamini mapumziko haya ya ligi tunaenda kufanyia kazi hiki tulichokiona, tatizo limeanzia mbali, hivyo ni lazima tulitibu haraka iwezekanavyo,” alisema Hitimana.

Alisema tangu mchezo wa ligi ya mabingwa dhidi ya Jwaneng Galaxy ya Botswana, hawakupata muda kufanyia kazi kasoro hiyo, lakini mapumziko haya wanaenda kutibu tatizo hilo.

Kwa matokeo hayo, Simba imepanda hadi nafasi ya pili ikiwa na pointi nne nyuma ya vinara Yanga wenye alama 15 huku Namungo ikisalia na pointi zake tano hadi wakati huu timu zote zikiwa zimeshuka dimbani mara tano.

## Yanga yaivutia pumzi Namungo

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imesema baada ya kupata ushindi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mara tano mfululizo, wako kwenye maandalizi makali ya kwenda kuivaa Namungo katika Uwanja wa Ilulu mjini Lindi Novemba 20, mwaka huu ili kulinda rekodi yao ya kushinda mechi kwa asilimia 100.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli, amesema kikosi hicho kilichopewa mapumziko ya siku mbili baada ya mechi dhidi ya Ruvu Shooting Jumanne iliyopita, kimeingia kambini jana, huku baadhi wakitwa kwenye vikosi cha vya timu ya taifa.

“Kwanza tunawashukuru sana mashabiki wetu wa Yanga kwa jinsi walivyokuwa wakijitokeza kwenye mechi zetu mbili za nyumbani ili kuwapa morali vijana wetu kupambana zaidi uwanjani. Zimekuwa mechi mbili zenye manufaa sana na tumevuna pointi sita ambazo zimetuwezesha kufikisha pointi 15 mpaka sasa tukiwa kileleni,” alisema Bumbuli.

Alisema baada ya mapumziko ya siku mbili, Jumanne na Jumatano, jana kikosi hicho kilitarajia kurejea tena kambini, lakini kikiwakosa baadhi ya nyota ambao watakuwa wanakwenda kutumikia timu za taifa.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >